

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

BELGUT CONSTITUENCY, HELD AT

KIPTERE YOUTH POLYTECHNIC

ON

12TH JULY 2002

constituency public hearings, belgut constituency, held at kiptere youth polytechnic on friday 12th JULY 2002

Present :

Commissioner Abubakar Zein Abubakar Chairman
Commissioner Hon. Mrs. Phoebe Asiyu
Commissioner Pastor Zablon Ayonga

Secretariat Staff In Attendance :

Irungu Ndirangu - Programme Officer
Anthony Oluoch - Assistant Programme Officer
Regina Mwachi - Verbatim Recorder
Abdulahi Jilo - District Co-Ordinator
Sheikh Hussein - Translator

Caroline Lang'at - District Co-Ordinator Kericho
Patricia Maritim - Office Assistant

Tola - District Co-Ordinator
Joyce Mutai - C C C
Geoffrey Chepkwony - C C C

Meeting started at 9:15 am with Com. Zein in the Chair. The prayers were led by Pastor Keter.

Speaker : Hapa tunataka kuanzisha mkutano wetu. *[inaudible]* Tafadhali muchukuwe viti tunataka kuanza mkutano. Na wale wanafunzi muliotaka kutoa maoni tunataka muje. Tafadhali wale ambao mumesimama kule muje muchukuwe viti tunataka kuanza. Wale mumesimama tunataka kuona mumeketi ili tuanze *[inaudible]* naam... *[inaudible]* tena huyo ametoa hii, sasa... *[inaudible]* sasa... Mama usitafute *[inaudible]* mimi nakuonya tu... *[inaudible]*. Oh... Oh... Wewe siunazikiza tuna-record-iwa pale... Oh... lakini nilikuwa ninatoa maonyo. Maonyo hapana kitu mbaya, kama natoa matusi ni ndiye kitu mbaya, iwe-recorded. Nadhani ungetukaribisha natuanze *[inaudible]* tena kuna ingine *[inaudible]*.

Caroline Lang'at : Okay tutaanza mkutano.

Speaker[s] : Unaona haisemi sana, niwewe husemi.

Caroline Lang'at : Okay tutaanza mkutano sasa na kabla hatuja endelea nitamuita Pastor Keter akuje atuongoze kwa maombi. Karibu Pastor Keter.

Speaker : Mpaka uiwashe hiyo, weka-on, rudisha juu

Pastor Keter : Natuombe. Tuombe. Baba katika jina la Yesu Kristo tunakushukuru tena asubuhi ya leo, na nikwa mapenzi yako, asante kwa ulinzi wako, asante kwa maisha ambayo tunayo wakati kama huu Baba tunapo anza huu mkutano wa leo. Tunakushukuru Mungu tunapo *[inaudible]* kutoa maoni mbali mbali kuhusu sheria za nchi yetu. Tunaomba Mungu utuogoe kwa kila njia tunaposema tunapo-record-i, na tunapotoa maoni kwa kila njia, tunasema Mungu uwe pamoja nasi kwa sababu yale yote ambayo tutakayosema yana toka kwako. Mungu tunakushukuru kwa ma-commissioners ambao wamewasili hapa, nasema uwaongoze na uwasaidie kwa kila jambo. Na kwa wale ambao wamekusanya siku hii, iwe siku hii, katika sehemu hii, tunasema Mungu uwasaidie pia. Tunakabidhi kila jambo mikononi mwako tunapo anza, hadi mwisho na ninaomba nikiamini katika jina safi ya Yesu Kristo. Amen.

Caroline Lang'at : Okay asante Pastor Keter. Kwa wale ambao wamefika nadhani nyote mume-register majina yenu kwa hiyo desk ilio pale kando. Aliye pale anaitwa Patricia Maritim. Atakuwa aki-register all the participants' wanao kuja katika hii mkutano. Kwa majina naitwa Caroline Lang'at District Co-Ordinator Kericho District. Asante, nitarudishia Commissioners halafu wataendelea na programme.

Speaker : Unaskia

Com. Ayonga : Hamjambo. Kwa niaba ya Commissioners wenzangu ambao tuko hapa mbele nataka kumu ita Chief wa area hii aje atukaribishe hapa kwake ndipo nita waambia tunafanya aje.

Mr. Benjamin Cheruiyot : Wageni ambao wamewasili, ma-commissioners kutoka ofisi ya Katiba Kenya. Ninachukuwa nafasi hii kuwakaribisha nyinyi katika hii kituo chetu cha Kiptere Polytechnic. Vile tunajua mumekuja kuchukuwa maoni kutoka kwetu ili wakati wa kutayarisha Katiba ya Kenya iwe hata sisi tumetoa maoni yetu. Na hiyo ni shukrani vile mulipanga na vile mumefika siku ya leo. Hiyo ni yangu na haitakua mengi ila tu nikukaribisha nyinyi katika hii kituo chetu ile tuendeleo na nyinyi. Ninafikiri watu wetu wakonjiani halafu kile mmoja atatoa maoni yake vile anataka. Kwa hivyo munakaribishwa natunasema asante vile mumefika. Asante sana. Jina langu ni Benjamin Cheruiyot mimi ni Senior Assistant Chief Area hii ya *Kalianguet?* Kiptere Location. Asante.

Com. Ayonga : Asante Bwana Chief kwa kutukaribisha hapa na wale ambao mumefika naona watoto wa shule wanakuja kutoka upande ule. Munaweza kujiandikisha hapo kwanza. Kila mmoja wenu ajiandikishe ndipo muje muchukuwe viti upande huu. Na kwa wale ambao wamefika nawakaribisha tena. Leo hapa tumekuja kuchukuwa maoni yenu na ningewaomba kwamba mujue kwamba hatukuja leo kuulizwa maswali na majibu. Leo tumekuja kuwasikiza nyinyi kwa siku zote hizi ambazo mumekaa mukisikia ya kwamba Katiba inataka kurekebishwa leo tuna muje mutuambie maoni yenu, yale ambayo munataka. Unapoitwa kusimama hapa unaitwa utoe maoni. Jina lako linapo itwa hatutaki uje utuambie story za ziku zilizopita, mzungu alikuja hivi, taabu za Kenya ziko namna hivi. Sote hawa tuliyo hapa ni wakenya na tunajua taabu hizo. Kitu sasa tunataka ni wewe kutuambia suluhisho ya taabu hiyo, jinsi ambavyo wewe unaona. Na tena wakati ambao uta toa maoni hayo unayatoa kama wewe au unayatoa kama kikundi kwa niaba ya kikundi na lugha ile ambayo unaweza. Lakini kabla hamujaambiwa, hatujawaambia tutafuata mtindo gani kwa kutoa maoni ningelipenda kuwajulisha kwa wale ambao niko pamoja nao na ndipo tuta ambia nyinyi jinsi ambayo tutakaka mfanye.

Kwanza kwa mkono wangu wakulia ni Commissioner Bibi Phoebe Asiyo. Nitakuja kumupa nafasi badaye awasalimie. Na mkono wangu wakushoto ni Commissioner Zein Abubakar naye badaye nitamupa nafasi awasalimie. Kule katika meza ile yule huyo mama amevaa miwani ni mama Regina. Mama Regina ametoka ofisi yetu kuu ya Katiba. Yeye atakuwa na kazi muhimu ile ya kunasa maneno munayotoa, ana kanda na ki-machine kule ambacho neno utasema ata kuwa analinasa hakuna neno litapotea. Hata ukikohoa atachukuwa kikohozi chako. Kule kando yake huyo ni Bwana Oluoch. Bwana Oluoch huyo yeye anaandika kama typewriter, anaandika kila kitu ambacho anaandika, na yule mama ananasa. Kwa hivyo hakuna neno lenu litakalo potea hata moja. *[inaudible]* Na kule juu, muangalie upande wenu wa mkono wakulia huko, huyu ambaye ameinua kitabu huyu ndio Programme Officer kutoka ofisi yetu, yeye atachukuwa kila Memorandum, yale maneno mumeandika, naona munamakaratasi hapo mumeandika, kusanya kila mmoja wao, kule ana-file ambayo ni ya chuma ambaye hakuna karatasi itakayo potea. Yeye anaitwa Bwana Irungu. Yeye anachunga hayo mambo. *[inaudible]* Okay, kwa hivyo yeye ana pia pahali ambapo utajaza, kuna-register ambayo utajaza jina lako kwamba umetoa-memorandum au kwamba umetoa maoni, yale ambayo unasema bila maandishi. Kwa hivyo kuna njia ambazo muta aambiwa ya za kutoa maoni. Na kwanza hebu mupate salamu kutoka kwa Commissioners wenzangu. Kwanza ni mama bibi Asiyo.

Com. Asiyo : Asante Pastor kunipa nafasi ya kuwa salimia watu wa constituency hii ambao wata hudhuria hapa Kiptere ili

watueleze maoni yao juu ya Katiba mpya ambaye itatusaida kujenga Kenya mpya. Tunajua kwamba Kenya inabahati sana kwa vile watu wa Kenya wametafuta sana Katiba huu mpya kwa miaka zaidi ya kumi. Na si kawaida kwa nchi nyingi ya Africa kutengeneza Katiba kama hakuna vita. Lakini hapa kwetu tumebahatika kwa maana Serikali pamoja na watu wote wakenya walikubali Katiba mpya iandikwe wakati huu ambao tuko na President ambaye yuko mamlakani wakati huu na hakuna mzozo wowote ilio mbaya zaidi katika nchi hii kwa hivyo tuna shukuru Mungu kwa hayo. Na tunatumaini ya kwamba nyinyi ambao mulifika hapa mutatusaidia na fakira njema ya kutengeneza Katiba mpya. Sisi kama ma-commissioners hatuko na uwezo wakuandika Katiba bila kupata ithini na maoni kutoka kwenu. Kwa hivyo tunawashukuru na ku wauliza tafadhali mtuletee mambo yatakayo tu saidia kuandika Katiba mpya. Asanteni sana.

Com. Ayonga : Asante mama Asiyu, sasa itakuwa Bwana Abubakar Zein.

Com. Abubakar : Habari ya asubuhi. Kama alivyo sema mwenyekiti wa kikao hiki, mimi naitwa Abubakar Zein na mimi ni mmoja kati ya ma-commissioner wa Tume ya kurekebisha Katiba na kwa ada na desturi zetu za kiafrica wazee wakisha sema mimi ni kukubali na kuafik na kuyapendekeza waliosema. Asanteni.

Com. Ayonga : Asante Bwana Abubakar Zein. Sasa katika kikao cha leo. Ninataka kumuuliza Bwana Abubakar Zein achukuwe wadhifa wa mwenyekiti. Yeye ndiye atawaambia taratibu ya kuchukua maoni. Sasa mpaka wakati tutakapomaliza yeye ndiye atakuwa mwenyekiti. Bwana Zein njoo uketi hapa.

Com. Abubakar : Asante sana Pastor Mzee Ayonga. Kama alivyo sema Mzee amenipa kazi ya kufanya na mimi nitajaribu kuifanya kwa uwezo yangu. Kwanza kabisa ningependa kuwapa maelezo kuhusu kazi ya leo tutaifanya namnagani, na kwa haraka kabisa nita waambia kwamba, wale ambao wamekuja hawajajiandikisha waende pale kwa lile dawati pale, kwenye meza ile ndogo alio kaa ule Binti, wajiandikishe pale. Wale watu wanaojiandikisha pale, wanajiandikisha kwamba wamefika na kuhudhuria kikao hiki. Na kuna watu aina mbili wanaojiandikisha pale. Wale ambao watatoa maoni leo, na wale ambao wata kaa kusikiliza tu. We are registering both observers as well as those who have submissions to make. Hilo ni la kwanza.

La pili, tutakuwa tukitumia ile orodha ya majina tukipata kutoka pale, tutakuwa tukitumia hiyo ili kuwaita watu jinsi walivyo jiandikisha. Aliyejiandikisha number ya kwanza ataitwa apewe fursa ya kwanza. Halafu nikuaambie ya kwamba sisi kawaida huwa tunajipa haki kama Tume, ikifika wakati kutakuwa kuna sababu za kutosha kutoka katika orodha hii ya majina. Kando kidogo kama kwa mfano tupate bibi ambaye ni mjamzito tuta jaribu kumpa fursa ya kuzungumza au mtu Mzee sana, au mtu ambaye ni mlemavu, au mtu mgonjwa, au mtu yeyote ambaye anasababu ya kutosha kupewa fursa ya kuzungumza mbele, hata kiongozi wetu yeyote hapa akitokea tutampa fursa azungumze halafu tutarudi kwenye orodha. Au si sawa hivyo? Ikiwa siwasikii na pengine munaona si sawa. Ni sawa hivyo? Sawa.

Lingine la muhimu kufahamu ni kwamba kuna njia tatu za kutoa maoni. Na njia zote hizi ni sawa.

Njia ya kwanza ni kwamba uwe na maandishi umeandika, kuna maandishi yako umeandika, na unataka ku yatoa bila kuzungumza. Ukiwa ni mmoja kati ya wakenya ambao wanataka kufanya hivyo, unakwenda, ukishajiandikisha pale unakwenda pale kwa yule Programme Officer wetu, unatoa maandishi yako, unaandika jina lako kwenye register, kwamba umetoa maoni kwa Tume ya kurekebisha Katiba. You don't have to wait for us.

Njia ya pili ni kwamba unamaanishi yako lakini unataka upewe fursa utaje mawili matatu yalio muhimu katika maandishi yako ili wenzako wajue ni mambo gani unapendekeza kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Ikiwa unataka kufuata njia hiyo hatutakuruhusu kusoma hayo maandishi. Hiyo memorandum hatutakuruhusu kuisoma. Kitu tutakachokupa ruhusa ufanye ni utushambulie yalio muhimu peke yake, Uguse tu muhimu useme haya ndio mambo ambayo nilikuwa ninataka kuyadokezea kwamba yamo katika memorandum yako. Sisi kama Tume tuna njia zetu za kusoma na ku-process, na kushughulikia memorandum hiyo. Maandishi yako ukiyatoa tutayashughulikia ipasavyo kama maandishi ya wakenya wengine.

Njia ya tatu na ya mwisho ya kutoa maoni ni kwamba wewe uwe huna maandishi lakini unataka kutoa yalio moyoni na kichwani mwako kwa kauli yako, kwa mazungumzo. Like you want to make oral submissions. If you want to make an oral submission, you will be allowed to do that, halafu hizo ndio njia tatu. Ukishaitwa jina lako tunakuomba uje hapa kwa microphone hii, kwa sababu alivyo sema Mzee Ayonga tuna-record kila kitu hakuna kitu ambacho hatutaki ku-record. Tuna record kila kitu. Uje, ukifika hapa kwenye microphone, utaje jina lako na uanze kutoa mapendekezo yako. Useme mapendekezo yangu haya!. Sasa ni jambo muhimu sana utilie maanani hili nitakalosema sasa. Kwamba ukiitwa tunajua mila na desturi na ada zetu kama waafrika, kawaida huja ukawatambua viongozi walioko hapo, ukawashukuru wageni, lakini leo tunataka kubadilisha mila hiyo. Hatutaki uje hapa useme 'tunapenda kuwashukuru ma-commissioners na tunapenda kupongeza commission hii kwa kazi inayofanya muhimu, namna hiyo uendelee, uendelee... napenda pia kumtambua Mp na Do na Assistant Chief, ukifanya hivyo dakika zako zimeisha mimi nitakuambia umemaliza kwa hivyo wakenya wakisikiliza maoni yako itakuwa kwamba wewe ulikuwa ukiwasifu wengine tu. Kwa hivyo sisi tunataka wewe uje hapa, mila hiyo leo tuisitisha, leo tu baada ya leo tutaendelea na mila zetu, uje hapa useme 'jina langu mimi ni fulani wa fulani, mapendekezo yangu kuhusu urekebishaji wa Katiba ni haya, moja useme... mbili...', na kama alivyo sema Mzee, sisi kabla ya kuanza kukusanya maoni tulikaa chini tukafanya warsha nyingi sana kujifunza mambo mengi kuhusu nchi yetu. Historia tunajua, matatizo yetu tunajua, kwa hivyo usije ukaanza kuzungumza kwamba siku hizi wazazi wanapata taabu sana kufundisha watoto na unajua hakuna kazi, kumbe mambo yako tunayotaka kutoa ni kuhusu elimu. Kwa hivyo ukija hapa useme mapendekezo yangu kuhusu elimu ni haya... kuhusu uchumi ni hivi... kuhusu Serikali ni hivi... kuhusu uchaguzi ni hivi... Na kila mtu atapewa dakika tano. Sisi tunafahamu kutokana na uzowefu wetu wa kazi katika mikoa mengine, na tumebakisha mikoa... tukimaliza hapa, tumebakisha mkoa mmoja tu Western tumalize, kukusanya maoni katika sehemu za uwakilishaji bungeni. Ukitumia vizuri dakika zako tano utamaliza hata kabla.

Lingine la muhimu ni kufahamu ni nini? Kwamba lugha gani itatumika hivi leo. Tutatumia lugha tatu. Lugha ya kwanza ni

Kiswahili, ambayo ni lugha yetu ya taifa. Lugha ya pili ni kingereza. Lugha ya tatu ni lugha ambayo inazungumzwa hapa. Hapa inazungumzwa lugha gani? Kipsigis!. Tutatumia kikipsigis kwa mtu ambaye anaona hawezi kuimudu lugha ya kiswahili au ya kingereza. Anaona atajieleza vizuri zaidi kwa kikipsigis, kutakuwa na mkaleman. There will be somebody to translate from Kipsigis to Kiswahili or English. Lakini ujue ukitumia mkalemani kwa sababu wewe ukizungumza halafu mkaleman azungumze time zinaenda hivyo kwa hivyo tuta kuangalia vizuri ukianza kusema maneno mengi sana tutamuaambia mkaleman muambie huyu Bwana atoe mapendekezo, utasikia. Utanisikia mimi kama mwenyekiti, nafikiri Mzee ameniambia leo niwe mwenyekiti kwa sababu damu ya ujana inachemka, inasema toa mapendekezo ukianza story nyingi nitakuambia je unapendekeza nini ndugu yangu. Nausisikie vibaya, au kuna mtu atasikia vibaya hapa? Hakuna.

Lingine la muhimu kufahamu ni kwamba lolote utakalo zungumza hapa unalindwa kisheria. Maanake nini. Maanake kwamba wewe uko uhuru kusema lolote unalotaka. Hakuna mtu atakaye kufuata baadaye au ofisi fulani ikufuate au Assistant Chief akufuate, hakuna. Unalindwa kisheria. Sheria inakulinda. Inasema wazi kwamba maoni yako unalindwa. Vile tunavyolindwa sisi ma-commissioners kufanya kazi zetu, na nyinyi munalindwa kisheria kutoa maoni yenu. Lakini hiyo haina maana kwamba unauhuru wewe wakuja hapa kumkashifu mtu au kumharibia mtu jina au kumtukana mtu fulani. Maoni yako utazungumzia mambo muhimu, issues. We are not going to make this a personal forum to attack other people or institutions. Sijui kama tunaelewana hivyo. Kwa hivyo hatutaki majina ya watu, tunataja mambo tunayotaka ya ingie katika Katiba. Sijui kama tunaelewana hivyo. Mpaka muniambie kwamba munaelewa ndio mimi niendele. Sijui tunaelewana hivyo? Ni sawa? Sasa kufikia hapo kawaida mimi huuliza je! kuna mkenya yeyote aliye hapa ambaye hakufahamu mambo haya au kuna kitu anataka afafanuliwe zaidi ana swali lolote hapa? Kuna mkenya mwenye swali lolote hapa? Hakuna mkenya yeyote mwenye swali? Kwa kuwa tunaona hakuna mtu mwenye swali naomba munipe ruhusa nianze kazi na kumuita mtu atakaye tufungulia kikao chetu leo kama alivyo sema mwenyekiti. Ningependa kukitambua kikao hiki sasa kuwa kikao rasmi cha Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya kwa minajili ya kukusanya maoni ya wakenya ile kubadilisha Katiba yetu. I would like to officially recognize this as an official sitting of the Constitution of Kenya Review Commission for the purpose of collection of views of our people to alter our Constitution. Sasa nikisha sema hivyo kwamba nimekitambua kikao rasmi kinanidhamu yake. Hapa pana kuwa kama kortini sasa. Watu hawapigi makofi, ikiwa mtu atatoa maoni uyafurahiye, yafurahiye moyoni kwako. Kwa sababu tuna-record kila kitu. Ukipata nafasi uje useme naunga mkono jambo fulani. Mtu akisema jambo ukasirike, kasirika ndani ya roho yako. Ikifika zamu yako uje useme jambo lile halikunifurahisha na pinga. Lakini huna haki ya kupiga kelele kumshangilia mtu au kumzoma mtu. Sasa namuomba Bwana Jeremiah Kirui awe mtu wa kwanza kutufungulia kikao hiki na Bwana Jeremiah Kirui unadakika tano.

Mr. Jeremiah Kirui Cheruiyot : My name *[inaudible]*...

Caroline Lang'at : Karibia...

Mr. Jeremiah Kirui Cheruiyot : Hallo, hallo...

Caroline Lang'at : Songa karibu na mic...

Mr. Jeremiah Kirui Cheruiyot : Hallo, hallo, hallo, hallo, hallo for my presentation I would like *[inaudible]* okay, I am Cheruiyot Jeremiah Kirui from Nagrio Self Help Group and I am presenting the following views.

That on the powers of qualities of the President: I am recommending the following: That the President should be elected directly from the people by the people and should not be an elected Mp and should have clean record and should not be suffering from any terminally ill diseases such as Cancer or Aids.

Powers of the President: Presidents powers should must be reduced drastically and demarcated to avoid confusion. The President should have powers to appoint Ministers, High Commissioners, Commander of Armed Forces Police and Attorney General but should not have the following powers. The President should be in a position to elect the Electoral Commissioners, Controller or Auditor General, Judges, Chief Justice or Permanent Secretaries, Chancellors of any University or to appoint anybody Head the Public Service Commission or Head the Director of the Parastatal Bodies.

Members of Parliament: They should be above thirty years of age, Degree holders, have clean development record, should not be suffering from terminally ill diseases, such as Aids, Cancer and many others. Should be mentally and morally upright. Should be a full time job. Should lead by consultation with the constituents. Should be recalled when he is out of that constituency for at least three months.

On issues of nomination: Nobody should be nominated as an Mp.

On Councillors should be above twenty-five years of age. Should be at least form four. Should be fluent in English and Kiswahili. Must have clean development record. Should not be suffering from any terminally ill diseases, Aids or Cancer and many other diseases. He /She should be open for impeachment.

Chairman of the County Council must be a Degree holder. Should be elected directly by the people must be thirty years and above. Must speak English and Kiswahili. Must have professional qualification especially that of Management and Administration.

On County Councils: County Councils or Local Authorities should be autonomous and independent.

Ministry of Local Government: The role of the ministry should be that of influencing the policies of the local authorities and should not direct as it is now.

Electoral Commission: Chairman of the Electoral Commission and Commissioners must be Graduates. They must be people of clean record honest and transparent in all aspects. Must be forty years and above. Must be selected by Parliament or the Commission of the Professionals formed by the Parliament.

Creation of Constituencies: Constituencies must be determined by the total number of people who should be at least twenty thousand. A Ward should have at least two thousand five hundred people.

Political Parties: Kenya should have at least three political parties to be sponsored by the State. Parties should have clear vision and democratic in nature. All parties should be treated equally by the State especially be given the opportunity and resources to sell their individual or party policies.

Gender equality: Boys and Girls be given equal treatment in the distribution of resources and opportunities of employment and education. Conducive environment for learning and development must be created for them. Men and women be educated to become better and excellent men and women. They should have a conducive environment in their place of work and home. Equality for men and women should be determined by freedom to complete in the contribution do what the development and growth.

Com. Abubakar : *[inaudible]* hiyo memorandum...

Mr. Jeremiah Kirui Cheruiyot : Yeah. Lastly, people with disabilities: The Government and State has the responsibility not only to protect the disabled but equally to provide for their basic needs such as food shelter and provide for health. The State should provide social amenities such as education, medication, and recreational facilities for them.

Last on issues of public health: The State should revert to the original method of supplying all the essential drugs and medical aids to hospitals, health centres and *shop?* health centres and those who are suffering from terminally ill diseases such as Aids must be treated free.

Com. Abubakar : Thank you very much Bwana Jeremiah. Asante hakuna swali na nivizuri kusema Bwana Jeremiah ame tumia exactly five minutes, alikuwa mtu wa kwanza si ku taka kumuuzia kusoma lakini ametumia five minutes exactly na sasa ameenda kujiandikisha pale. Na ni zuri kwamba umesikia nikiuliza ma-commissioner wenzangu kama kuna swali lolote, ikiwa unakuja kutoa maoni hapa mmoja wetu anaweza kuwa na swali la kukuuliza ufafanue jambo. *[inaudible]*... Kuna watu ambao wamekuja hapa wanakuja kukaa hawajajiandikisha kule. Tunaomba waende pale kwenye ile meza yule Binti anayefunga mikono mwenye kalamu ya blue anaandikisha list. Ukijiandikisha kwenye list ndio tutakuita jina. Hizo list ndio tunatumia kuitia watu majina. Sasa mtu wa pili ni Josiah Surum. Bwana Josiah Surum karibu nafasi ni yako. Uanze unadakika

tano kama mwenzako.

Mr. Josiah Surum : Mine is to give... I am Josiah Surum I come from Belgut Youth Model Business Project.

Education be made free from Standard One to Form Four and University be free and fully subsidised to enable poor families afford education for their children.

Kenya school equipment scheme be revised to enable majority from poor schools get quality relevant equipment which can enable them compete equally. *[inaudible]* Yes.

Employment: Employment must be guaranteed to all Kenyans who are able and willing to work.

Unemployment: Should go with benefits. The State should create a security van which caters to the needs of unemployed people. A model payment of ten thousand to an undergraduate degree holder. Six thousand for Diploma holder and Four thousand for Form Four who are qualified. This should not make anybody denied of his or her normal life.

So on the question of experience for requirement of employment is about an ill modification. This has denied a majority of qualified Kenyans to secure their rights total and better living. So on those issues I hope the Commission will see whatever they will do.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Surum. Umesema vizuri umemaliza mambo yako kwa muda unayofaa. Uende pale kujiandikisha na utoe hiyo memorandum tutaitumia, tutasoma kila kitu hapo natutumie hiyo katika kazi yetu. Asante sana. Tunamuomba Bwana Philemon Mabwae. Mzee karibu

Mr. Philemon Mabwae : Sijui kama mimi niko mfupi. Hii itakuwa sawasawa. Yangu. Yangu ni. Jina langu naitwa Philemon Mabwae Mzee ya area hii. Basi sasa yangu haita kuwa nyingi.

Ningependa kuongea juu ya Majimbo: Yaani sasa tunataka Serikali ya majimbo ambaye kile province ijisimamie. halafu wanachagua President yao. Halafu mwisho kwa hii majimbo wanachagua Prime Minister. Halafu yaani kutoka kwa ile Serikali ambaye ina shinda. The winning party. Yaani sasa the winning party watachagua Prime Minister.

Lingine nikiendelea kwa area hii yetu tukonashida kubwa sana. Ningependa watu wana kunyua pombe. Yaani wakishikwa, siku moja nilitembea pande ingine nilikuwa nimetoka kanisa halafu nikazungumza na mama mmoja naona polisi wakaja kushika wale walevi na mimi nilikuwa mimi na kunyua chai halafu sasa hawa watu wanaanza kuchukua yule mtu ambaye anatoka kanisa. Lakini mimi nataka sasa tuanze tribunal ile ya zamani. Sijui inaitwa tribunal. Yaani kitu namna hiyo tribunal hiyo kama ya

zamani kwa sababu sasa badala kuchukua mkristo ama muhubiri aende kulala kwa remand na yeye alikuwa ana hubiri sasa hiyo imekuwa shida kabisa. Inatakikana iwekwe sheria kujua ya kwamba yule mkristo ambaye anahubiri, kama anapata mlevi halafu wakati mwingine na kamata pombe kidogo kwa jerry can ile ndogo ndogo achukue nasema nilikua na lewa, kwa hivyo Serikali yetu ningependa ya kwamba utusaidie kwa hapo.

Lingine yaani sasa iko mambo ya President. Nime sikia chama nyingi. Sasa mtukufu Rais wetu, sasa iko age. Nimeona ya kwamba wako wengine ambaye iko na rika moja kama inazuia sasa President kama President ingine ambaye iko generation ya yeye kama yeye, kama sasa anataka kua President ni afadhali President yetu aendelee kuliko sasa Mzee mwengine apigania President.

Com. Abubakar : Tumejua...

Mr. Philemon Mabwae : Umeelewa kabisa. Yangu hi hiyo tu.

Com. Abubakar : Asante sana Mzee wangu. Mzee amefanya jambo nzuri. Umeona Mzee sikumuingilia alipo sema hadithi ya pombe. Uende pale ujiandikishe Mzee. Na heshimu miaka yake, lakini ametumia dakika tatu hakutumia dakika tano, tatu peke yake. Sasa naita Charles Maiwa? Charles Maiwa? Karibu Bwana utaje jina, uinue microphone kidogo, usongelee karibu kabisa. Songea karibu na mic, utaje jina uanze.

Mr. Charles Maiwa : My names are Charles Maiwa Project Manager wa Kiptere Youth Polytechnic. I am presenting a memorandum on behalf of the staff of this particular institution.

Ningetaja tu major points lakini, what I could read are self explanatory in the papers. First of all this is, I am saying some few things.

Youth Polytechnic Instructors should be defined recognized and be absorbed in the Ministry like any other Civil Servant. The Government absorbs and recognize the presence of staff in the Youth Polytechnic like any other Civil Servant.

To set up a system of paying salaries: For staff in the Ministry for now there is delay of grants. Salary is in payment per month is first of all through grants. The salaries to be paid by the Ministry not the grants.

Two. Recognize the Basic Salaries by Job Groups:

Three: The staff to be provided with House Allowance, Staffing Allowance, Medical Allowance, Hardship Allowance and Scheme.

Lastly: The Government should extend Bursary Funds to Youth Polytechnic Students.

Finally: I want to say that... most of what I could have said is actually self explanatory in the paper.

Thank you very much.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Charles kwa kuwa very precise. Philip Keter? Bwana Philip Keter nizamu yako sasa. Na kama mutanipa ruhusa wakenya wenzangu niwe naita mtu mara mbili ikiwa hayuko niende kwa jina linalofuatia. Au si sawa hivyo? Philip Keter, mara ya kwanza, Philip Keter, mara ya pili. Hayuko Wilson A. Chepotungo. Karibu Mzee, karibu Mzee. Utaje jina na uanze kutoa maoni yako. Mzee yangu.

Mr. Wilson A. Chepotungo : Jina yangu ni Wilson...

Com. Abubakar : Songea kidogo karibu na mic Mzee.

Mr. Wilson A. Chepotungo : Wilson Chepotungo, sasa mimi na sema tu kitu moja. Na rudishia yeye Mzee Moi anaendelea na kazi yake.

Ya pili nataka nini, ile Assistant Chief na Chief nataka wafanye kazi. Kwa maana zamani alikuwa muingereza alikua na andika hawa. Nataka chungu mwaafrika yote. Kwa maana kama hapana wacha, nawaacha hawa Assistant Chief na Chief halafu na potea kwa dunia, dunia hapana kuwa mzuri. Nataka namna hiyo.

Ya tatu, sasa nataka kila mtu nakaa kwa nchi yao. Sitaki mwingine na kuja haribu maneno ya wengine. Kwa maana Mungu alijua sababu alikuwa anatenganisha watu mbali mbali.

Hapo hapo hapo tu maneno yangu yanatosha ndio hapo.

Asante sana.

Com. Abubakar : Ngoja Mzee, Asante sana Mzee, kuna swali hapa, kuna swali Mzee, Mzee rudi kuna swali Commissioner anataka kukuuliza, asante.

Com. Asiyu : Mzee unasema watu wakae kwa miji yao wenyewe...

Mr. Wilson A. Chepotungo : Yeah!

Com. Asiyu : Unaweza kufafanua zaidi? Hiyo ni mambo ya majimbo au ni mambo gani?

Mr. Wilson A. Chepotungo : Hii ni mambo ya kutokea zamani alikuwa na kusema nataka tu wenyewe wakuweko.
[inaudible] Mimi nasema namna hii zamani, si alikua iko nchi yao, kwa kila mtu nani alikua na aanzia hapo

Com. Abubakar : Mzee unataka kusema kwa kikipsigis?

Com. Asiyu : Sema kwa kikipsigis ndio basi...

Mr. Wilson A. Chepotungo : *Amwae alelen in.....*

Com. Abubakar : Ngoja basi, ngoja... nani ata tafsiri? Shika hiyo mic, ile ingine, ile ingine, ile yenye black. Shika hii.

Translator : Hii

Com. Abubakar : Halafu akisema wewe una...

Translator : Hebu weka on!

Com. Abubakar : Sema Mzee, endelea

Mr. Wilson A. Chepotungo : *Amwae alelen in amune si bik che kimiten en koren nywan koma nyalu kobur en koren nywan I?*

Translator : Mzee anasema

Com. Asiyu. : Weka on.

Translator : Anasema kila mtu akae kwake.

Mr. Wilson A. Chepotungo : Haya sasa mimi nasema tu namna hiyo.

Com. Asiyu : Okay

Mr. Wilson A. Chepotungo : Unaelewa.

Com. Abubakar : Asante

Mr. Wilson A. Chepotungo : Asante

Com. Abubakar : *[inaudible]*. Bwana Jael, Joel K. Kirui? I think... Japheth Rono? Kiptere Polytechnic staff member. Benjamin Cheruiyot? Benjamin Cheruiyot? Korrir Shadrack? Shadrack Korrir? Niwewe kijana? Njoo, njoo. Shadrack ikiwa ni wewe uje utaje jina ni mwanafunzi wa kutoka wapi na utaje uko katika darassa gani.

Mr. Shadrack Kiptoo Korrir : Kwa majina naitwa Shadrack Kiptoo Korrir. Mimi na soma katika hii institution ya Kiptere polytechnic niko katika darassa la Mvm, Motor Vehicle Mechanic. Niko na maoni haya. Nitayasoma kwa lugha ya kingereza.

The Constitution should provide for gender equality as a basic principal in preamble and substance of the Constitution. Generally the relevant stake holders should assist in coming up with the best way of protecting human dignity is fundamental rights and freedom for all.

Ni hayo.

Com. Abubakar : Asante kijana uende pale ujiandikishe kwamba ume toa maoni kwa Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya. *[inaudible]* Asante sana naomba Bwana Kipkoech Lang'at? Kipkoech Lang'at? Njoo uje ufanye haraka, utoe maoni yako, utaje kama mwenzako alivyo sema utaje polytechnic yenu, unafanya nini, nauendeleo kutoa maoni.

Mr. Kipkoech Lang'at : Kwa majina yangu mimi naitwa Kipkoech Lang'at mimi natoka shule ya Kiptere.

Kwa maoni yangu: Children's rights should be observed in learning institutions and even our homes where children's needs should be catered for. Whilst there virginity be respected. To cater for these children law courts should be established.

Com. Abubakar : Asante sana ujiandikishe pale. Moses Cheruiyot? He is a student also Moses. Wale wamejiandikisha kama observers na waruka. Wale walisema wanakuja kusikiliza tu, simuiti lakini ikiwa kuna wakati umefika unajisikia unataka kubadilisha useme maneno uende uzungumze na yule dada au Co-Ordinator useme mimi nataka kubadilisha. Endelea Kijana.

Mr. Moses Kipkorrir Cheruiyot : My names are Moses Kipkorrir Cheruiyot. I am from this institute of Kiptere Youth Polytechnic and I am in the section of masonry. I would like to present the following views.

About Bill of Child Rights: Children should be catered for by the Government to get basic education and materials both in primary and technical institutions. They should be provided with free medication on children under eighteen years.

That is all.

Com. Abubakar : Asante sana ujiandikishe pale. Sasa namuita Florence Kipngetich? Florence sasa nizamu yako.

Ms. Florence Kipngetich : My names are Florence Kipngetich from this institution. My opinion is this.

Children from technical institutions, recognized sources or sub lined marginal tribes are entitled to learn.

Thank you.

Com. Abubakar : Asante Florence ujiandikishe pale. Anayefuatia sasa ni Julius Cheruiyot? Julius Cheruiyot karibu. Nizamu yako Bwana.

Mr. Julius Cheruiyot : My names are Julius Cheruiyot from Belgut Constituency. *Sosiol?* Location

System of Government: I propose a Federal type of Government in terms of management of Government we should have separation of powers. That is Executive Judiciary and Legislature must be given separate roles and duties and functions and each be independent.

Powers of the President: Be reduced also and members of Judiciary like Chief Justice be proposed by the Parliament.

Public service: I also propose that recruitment exercise be given issues on merit not people be given chances because you are somebody known by a boss or someone.

In terms of marginalized groups: I also propose that full rights of citizenship be given to minority groups like *Okieth?* we also have women be given their rights. Children and the disabled.

Citizenship: Also is very important and every citizen must be given medical services with free education and also employment even political freedom be given to every citizen.

In terms of Policy making: Citizens must also be given rights to determine major policies like even salaries of the

Parliamentarians and other major issues.

Talking about Local Government: I say that County Councils be given powers to determine affairs like financial and social. Mayors and Chairmen of Municipals, Cities and County Councils be elected directly not by Councillors or appointment.

Resource Management: We also have land and natural resources which have been misused in some way or another. So I propose that County Councils play a minor role in allocation of land. People of that particular Location or locality where we have resources like land or minerals be given a chance to determine the share or utility of those resources. Minerals which are also mined from a particular area be taxed so that they are utilized by the people from that locality.

Corruption Issues: Abuse of office must be tackled seriously. In terms of handling corrupt cases an Anti-Corruption body should be established and be given powers to investigate and actually determine judgment of such corrupt persons.

Ombudsman: Office of the Ombudsman be established to help the public in routing out corruption.

A court should be also established so that it can help the poor, the court which will not be charging any amount in the way of fees to help the poor, in interpretation of law and also in following up cases. Handing penalties should also be maintained on serious criminal cases, like murder.

Lastly I propose that the Youth be given chances in terms of management of offices in public services and in any other area.

Thank you very much.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Julius. Hiyo memorandum uipeleke pale utoe kwetu na u-sign register yetu kwamba wewe umetoa maoni kwenye Tume ya kurekebisha Katiba. Bwana Joseph Kiptum Koech? Karibu Bwana.

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Asante sana. Jina yangu ni Joseph Kiptum Koech mimi natoka *Kathiong'et?* Location Belgut. *[inaudible]* kwa sababu mimi ni mfupi kidogo. *[inaudible]* Mimi natoka *Kathiong'et?* *[inaudible]* Jina yangu ni Joseph Kiptum arap Koech kutoka *Kathiong'et?* sub Location, Belgut Division. Maoni yangu ile nime andika kidogo kwa kingereza.

Peopled participation in Public Affairs: People at home should be the ones to discuss about their affairs and salaries or their Mp's.

They should be allowed also to discuss about the land issue. Ukisema nikitafsiri kwa kiswahili tunashida ya mashamba ya

wazee ya zamani wale ambaye walipoteza, pengine Mzee alipoteza... hakuwa na kipande, alipoteza kipande na iko na Land Transfer. Hii tungeweza kuwaachia wazee wa kijiji na Chiefs kwa sababu hawa ndio wanajua. Kuliko kumuambia atafute kipande au atafute Death Certificate na huko zamani ili kua hiyo maneno hapana iko. Tukiwaachia wazee.

Com. Abubakar : Unataka mambo ya ardhi au *[inaudible]* wazee..

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Waambie wazee na Assistant Chief.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Distribution of land and natural resources : iwe kwa pahali hiyo vitu ili tokea kama County Council au kijiji hiyo wa-mange mali zao.

Ingingine ni mambo ya hii pombe ya kienyeji brewing: Kwa maoni ya wazee ambaye nimetembea nao wanasema hii maoni ya pombe ya zamani ya kienyeji, traditional drinks iwe-allowed. Halafu ma-chief wapeane mabarua kwa sababu hii mambo ya kuiba iba ndio inafanya watu wanalewa zaidi. Hiyo ni maoni ya wazee.

Com. Abubakar : Nasema hiyo sio kazi ya chief sasa una sema pombe ya kienyeji ihalalishwe.

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Ihalalishwe...

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Okay...

Com. Abubakar : Lakini ili ingine ya kuongezea *[inaudible]*

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Okay. Tena ingine ni kwamba maneno ya ma-chief ile ya zamani, ile Chiefs Act irudishwe ikae kama zamani...

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Halafu hawa wawe na nguvu zaidi...

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Joseph Kiptum arap Koech : Nafikiri kwa maoni yangu hayo machache nimemaliza.

Com. Abubakar : Asante sana Mzee. Uende pale ujiandikishe nautoa hiyo memorandum tutaisoma vizuri kabisa. Namuomba Bwana Peter Kitur? Bwana Peter Kitur? Oluoch kama unaweza kumsaidia Bwana Kitur uumpe mic ikiwa itamfikia pale. Hii ya wire. *[inaudible]* subiri kama, maanake kuna hii mambo ya kuzunguka huku chini, kama akikuletea hapo nafikiri itakua si vibaya. Bwana Kitur utaje jina lako halafu uendelee.

Mr. Peter Kipkoech Kitur : My name is Peter Kipkoech Kitur natoka katika sehemu ya Kiptere market. Ninataka kutoa maoni yangu kwa kingereza. *[inaudible]* My name is Peter Kipkoech Kitur. My name is Peter Kipkoech Kitur from Kiptere market. Mimi nataka kutoa maoni yangu kwa kingereza.

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Peter Kipkoech Kitur : Government: Government must be in Majimbo.

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Peter Kipkoech Kitur : President: President must be elected by the people of Kenya not from somebody to promote.

Education: From Standard one to University must be free.

Health: Hospital must be given free.

Administration: From Pc to Assistant Chief must be elected by the people.

Disabled: People should given free funds, their children and to be fed and to be given some money for their health by the Government.

Police case: Arrest must be ordered by the Judge. Anybody crime or corruption even if it is President Police should be... atatoa inje na kuweka kwa... jailed and Government... and not given any other jobs in the Government.

Ingin ni Judges: Judge should have free of worship without following up by the Government.

Hiyo ndio maoni yangu asante sana.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Kitur. Huyu kijana ata pokea hiyo uruditu pale ulikuwa umekaa ukae Bwana Ndirangu atakuletea ile register using pale pale. Kwa hivyo Bwana Kitur, Bwana Kitur subiri kuna swali kutoka kwa Commissioner pole.

Com. Asiyu : Ningependa kukuuliza Bwana Kitur kama una maoni yeyote ambayo ungependa tuaandike kwa Katiba iwe ya wale wasiojiweza?

Mr. Peter Kipkoech Kitur : Nilitoa Disabled people: Should be given free funds...

Com. Asiyu : Okay, okay. Thank you.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana

Mr. Peter Kipkoech Kitur : ...and free education and give the money for health.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Kitur. Uruditu pale ulikuwa umekaa, sasa Bwana Ndirangu atakuletea maandishi pale. Sawa. Nadhani hiyo list imeisha. Tunaenda kwa ya... Bwana Joseph Mabwae? Si alikuwa amezungumza Bwana Mabwae? Haya huyu ni mwingine Bwana Joseph Mabwae? *[inaudible]* Najua. Catherine Chumo? Catherine Chumo? Fredrick Metet? *[inaudible]* Ku-arrange nini Mzee? Ku-arrange nini? Oh! niwewe uki rudi basi inua mkono basi halafu nita kuona. Wewe unaitwa nani Mzee? Ukifika, uki rudi ukiwa tayari nifanyie hivi nita kuona. Haya Mzee. John Maiwa? Sawa. Benjamin Ngetich? Benjamin Ngetich? Karibu Mzee, karibu Mzee. Utaje jina uendele.

Mr. Benjamin Ngetich : Asante sana sijui nitafaulu kiswahili. *[inaudible]* Natosha? Asante sana nime fika hapa sijui nitafaulu kwa kiswahili kwa sababu kiswahili yangu ni ile ya zamani ya wazee ya zamani. Lakini nita jaribu. Asante sana kwa maoni ya Katiba mimi naitwa Benjamin Ngetich natoka *Shikawe?* Division yetu hapa chini mpaka *Chemabul?* yote namna hiyo. Na mimi Mzee ya health ya Kipsigis. Maoni yangu ni hii.

Na taka ya kwamba Katiba kweli tunataka iwe sasa, mimi na zungumza mambo ya Kanisa ipate uhuru, kila kanisa ya kila mtu apate uhuru. Kama watu wanapata saa ya kuabudu watoto wasiruhusiwe kutoka kuja kukimbia kimbiba, natakiwa aombe sababu inatakikana namna hiyo. Uhuru inatakiwa kila kanisa afuate sheria yao. Afuate sheria kama watu wa Jumapili, afuate sheria ya Jumapili ku swali bila kuja kukugusa na watu ambaye wana pumzika Ijumaa ama Jumamosi tena apumzike ya kutosha.

Sababu hapana kuja kuruhusia watoto shule amuruhisie kuja kimbiba kimbiba hapana kupumzika siku ya Sabato au siku ya Jumapili watu ili anipe mamlaka ile watu kuabudu Mungu.

Na tena sheria ingine naweza kuongeza hapo tena ni forest Unajua forest kama watu wanakata mpaka na kwisha maji inje itakuwa kavu. Inataka kuchunga kwa sababu miti ikiwa na forest tutapata mvua ya kutosha. Maji isiweze kukauka iwe dukani bure. Hafai Serikali hafai kuchunga forest kawaida. Kwa sababu misitu ni kama loudspeaker yetu zamani. Ukikata miti huko anaitika ndi, ndi, ndi. Lakini kama nchi inakauka hapana weza pata loudspeaker. Loudspeaker yetu ya zamani ilikua miti. Mtu akipiga kelele huko unaskia Oh!, Oh! ndio mambo tunavyo sema inafaa tuchunge forest yetu halafu tupate maji chemi, chemi ya maji watu wafaidike kwa maji.

La ingine hapana tena kwa ofisi hii mambo yote ya kinyumbani hapana kama kweli kama mashamba wazee ya nyumbani atatue kwa kinyumbani na hii badala ya kupeleka maneno huko mbele afae ajue nyumbani tuone vile namna gani.

Tena watu wa bunge kama iko juu huko hapana nauliza sisi watu wa chini halafu na peleka huko baada ya kuanguka kupeleka huko bila atatue mambo huko. Tutatue mambo ya mashamba kwa nyumbani wazee aelewe sawa sawa vile namna gani. Wazee watafaulu kwa sababu hujui mambo ya shamba na jua *sheria?* una pigana na nani wazee ndio wanaweza kutatua hiyo. Na wewe unaanza kuona vile namna gani.

Kwa hiyo sasa yangu pengine wacha ni *karani?* yangu bado kuja ya health tuseme ya youth tunataka amani kwa nchi hii. Lakini youth ana tu zungumzia mambo ya amani kutoka zamani mtu anaweza toka Maragoli natoka huko wapi, ili kuwa mambo mazuri. Unajua watu wa wabeberu watu walikua wanataka kwenda mpaka kule Nakuru tulikuwa tunapata pass ya kwenda naye kufika unaweza ona Oh kumbe unaenda. Kama Narudi unaweza pass hiyo hiyo. Ilikuwa tunapata hiyo namna hiyo. Lakini siku kama tunasema uhuru bure tunataka majimbo kwa kile mtu kama natoa boma yako uende kwa majimbo kila mtu afaulu majimbo yake, akae majimbo yake, kwa area yake, lakini sasa kama na tuko huko tena kugusa kitu yako urudi. Kama nataka kupita unaweza pata hata pass ya kwenda naye kurudi unaweza kuona kama sawa. Hiyo nafikiri ina weza kuchungwa nchi inaweza kuwa mzuri. Lakini kama watu wanaenda fuwaa ni mbaya.

Very good nafikiri na kwisha hapo.

Com. Abubakar : Asante sana Mzee, ngoja Mzee, ngoja, ngoja subiri kuna swali, halafu ukisha jibu swali uende kujiandikisha kule juu.

Com. Asiyu : Mzee umependekeza habari ya Serikali ya majimbo...

Mr. Benjamin Ngetich : Ndio...

Com. Asiyu : Na pia umesema kwamba watu wasi ingie kwa basi au magari mengine ku pita pita kwa mahali ya watu

wengine. Nataka ufafanue kwa maana Kenya ni moja na watu watakuwa wakisafiri kutoka upande moja mpaka ingine, kutoka Maragoli kupitia nchi ya Kalenjin mpaka kufikia nchi ya Kikuyu au nchi ya Jalu au nchi ya Mombasa. Unasema namnagani?

Mr. Benjamin Ngetich : Mimi nasema hapo...

Com. Asiyu : Nataka kujua...

Mr. Benjamin Ngetich : Ataweza kweli mtu akae na kama anataka kutoka... anataka kupita kwa...

Com. Abubakar : Ngoja Mzee

Mr. Benjamin Ngetich : Sisi tuko Kenya...

Com. Abubakar : Ngoja Mzee, ngoja Mzee

Mr. Benjamin Ngetich : Ehe!

Com. Abubakar : Kama nimemuelewa Mzee amesema hivi. Wakati wa ukoloni ilikuwa ukitaka kwenda nchi ya, mahali kwa watu wengine unapewa pass.

Mr. Benjamin Ngetich : Ehe!

Com. Abubakar : Mzee anasema watu waende, lakini wapewe pass. Hivyo ndio unasema...

Mr. Benjamin Ngetich : Kama ukisha toka kwa boma yako, kwa sababu kama mimi niko kijijini hapa kweli kama unataka kupita mbali naenda kuuza kitu yangu naweza kupata kutoka ile permit wale wanaweza kusoma Oh unaenda kweli kama siku Narudi unaona kama wewe uko na hiyo inaweza kuwa mzuri. Mimi sikatai kutembea na Kenya yote. Naweza tembea lakini naweza kuona vile kitambulisho gani unatoka wapi. Hiyo inaweza kuwa safi.

Com. Asiyu : Lakini hii ya Identity Card hapana tosha...

Com. Abubakar : Ya Kenya...

Mr. Benjamin Ngetich : Kenya gani wewe na sema hiyo...

Com. Abubakar : Kitambulisho...

Mr. Benjamin Ngetich : Ehe!

Com. Asiyu : Kitambulisho...

Mr. Benjamin Ngetich : Ehe! Sio kitambulisho. Mimi nasema muhimu kitu ambaye unaweza kwenda kuuza, lakini kitambulisho mimi ninaye kweli inaweza kutosha lakini kama yule atakwenda saa ngapi kitu unauza naweza una kama hiyo ni kweli. Hii kitu wewe unatoa vile ng'ombe yako ni safi..

Speaker[s] : *[inaudible]*

Mr. Benjamin Ngetich : Hapana sawa

Com. Abubakar : Sawa Mzee. Uende pale juu ujiandikishe Mzee. Sasa ningependa kutambua kufika hapa kwa bi Do ya hapa. Madam Do sisi tulianza na Assistant Chief wako akatukaribisha vizuri, tukaanza tumekuja ma-commissioner watatu wa Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya. Madam mweshimiwa Phoebe Asiyu ambaye nadhani unmfahamu na Mzee Ayonga Pastor ametoka kidogo na atarudi. Kama tunaweza kukupa fursa useme machache kabla hatuja endelea.

Ms. P. A. Dola : Commissioner, Honourable Commissioner Phoebe Asiyu na wenzake, wazee na viongozi mbali mbali ambao wako hapa, hamjambo. Sita sema mengi ningependa tu kuwakaribisha Sikowet Division na muendeleo na kazi yenu kwa hiyo mumekaribishwa na m-feel at home. Mumekaribishwa zaidi asanteni.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Do mimi naitwa Abubakar Zein na tutaendelea na kazi. Asante sana. Naomba kumuita Bwana Kennedy Nyakundi? Bwana Kennedy Nyakundi? Unaweza kuketi tu. Hapa kuketi tu. Utaje jina nauendeleo.

Mr. Kennedy Nyakundi : Kwa jina naitwa Kennedy Nyakundi natoka tarafa ya Sikowet na Location ya *Koliongwet?*

Com. Abubakar : Endelea

Mr. Kennedy Nyakundi : Natoka, natoka katika tarafa ya Sikowet katika sub-Location ya *Koliongwet?* Niko na machache ambao nataka kusema. Ukisema kweli nashukuru nimepata fursa kama hii kutoa mawazo yetu kuhusu Katiba yetu, na sisi wenyewe ndio tunataka tutoe wenyewe tunajitolea nani anatutengenezea Katiba.

Kwanza kitu nataka kuuliza maslahi ya watoto tuta weka wapi, kweli, watoto wameteseka miaka nenda miaka rudi. Kwanza nataka watoto wapatiwe maslahi yao, wachungwe kwani tunaona watoto wanateseka, kwanza tunaweka kuona watoto kama chokora. Chokora unawakuta hawajui wazazi ni nani, wazazi wao ni nani hasa. Wanataka wachungwe na Serikali.

Ya pili, tunapata kwamba hata vijana ambao wamemaliza shule hawana kazi ya kufanya, nataka Serikali yenyewe ichukue hatua, kama ni lazima Serikali ione kama ni lazima wanafunzi ama watu wa vijana wako nyumbani wa lazimishwe kuenda katika chuo fulani kuchukuwa maarifa ile waje kujitegemea. Unaweza kuta mtu amekaa barabarani hata watu wanashangaa, hakuna kazi, ukiuliza wanaenda kuambiwa mbona unakaa unaona mpaka wengine wanaenda kunyua pombe wana kunyua madawa za kuleviya...

Com. Abubakar : Sasa Kennedy hayo sisi tunayafahamu vile unajua wewe, ni mambo ambayo kweli yanasikitisha na mambo ambayo yana wapa watu shida. Lakini unataka tufanye nini.

Mr. Kennedy Nyakundi : Ningetaka Serikali yenyewe ijaribu juu chini kutafutia hayo pahali ya kujificha ama kufanya kitu ya maana.

Ya pili ni kuhusu walemavu. Unaweza pata mtu kama mimi hata yule, mimi ni afadhali kidogo naweza kutembea. Unaweza kuta, ndio unaweza kuja ni mukute mkubwa naweza muambia nisaidie nita fanya nini. Ana kuambia hakuna, sasa uta kaa mpaka lini. Unataka uombe msaada saa yote saa yote, hata nikikuja kwako saa yote saa yote ku kuomba msaada utasikia je...

[inaudible]

Mr. Kennedy Nyakundi : Kwa Katiba mimi nataka kama hata ni percentage fulani tupatiwe kazi, kazi. Ya pili tunataka pia viwete wapatiwe nafasi kuwa viongozi hata katika Parliament hata kuwa Rais. Lakini unaweza kua una akili lakini mguu hauna lakini unaweza fanya kitu yenye hata mwenye anao mguu hawezi fanya.

Ya tatu tena unaona wamama wanateseka wenyewe. Nime kaa, mimi na vumilia kweli naangalia wamama wako na taabu. Ukiangalia mama ndio ana fanya kazi...

[inaudible]

Mr. Kennedy Nyakundi : Wakina mama wanataka pia hao wapatiwe haki yao..

[inaudible]

Mr. Kennedy Nyakundi : Mimi najua ni kweli ni shida lakini nataka sisi tutatue yenyewe...

[inaudible]

Mr. Kennedy Nyakundi : Si ndio nataka kwamba wamama wenyewe hata hao wapatiwe nafasi, hata vijana hata hao wapatiwe nafasi.

Ya pili education. Education nataka system ya zamani and it should be free.

Another thing is that unakuta ndio, tuko na taabu mingi, tunajua kwamba Kenya iko na, uchumi ni mbaya lakini tujaribu sisi wenyewe tujitatie wenyewe. Na kwa hivyo mimi najua hata kama tuna lia hakuna uchumi ni mbaya lakini wale wenye wali fanya mambo ya ufadhili kuiba pesa wachukuliwe hatua kali.

[inaudible]

Mr. Kennedy Nyakundi : Kufungwa, hata ile mali wali iba warudishe ili hata sisi tujikokote. Kuliko kukaa tu idle... Ehe!

Haya basi tena ya pili yenye mimi naona, wenye hawafanyi kazi, wenye hawafanyi kazi ambao wame kaa... unaweza patia muda ya... nataka Serikali yenye inakuja ione ya kwamba, muda tuna patia mtu muda, unaambiwa tume kupatia kazi, fanya muda kwa miaka kumi utoke mwengine aingie.

Ya mwisho tena ni...

[inaudible]

Mr. Kennedy Nyakundi : Hapana, si niko na... Haya freedom of worship. Worship unaona kwamba kuna kiwango. Tunataka kusema madini fulani, lakini dini ya mambo ya masheitani out. Devil worshippers out.

Com. Abubakar : Asante sana

Mr. Kennedy Nyakundi : Sawa

Com. Abubakar : Asante sana, Bwana nani Oluoch msaidie hapa. Asante sana Bwana Kennedy uende pale ujiandikishe kwenye ile meza pale. Asante Kennedy. Sasa Bwana Philemon Kireni? Bwana Philemon Kireni? Karibu Bwana.

[inaudible] because of the list... kama unaweza kumuteremushia tena hiyo kidogo. Bwana Kireni subiri kidogo. Kaa tu

usubiri nitakuambia useme. Nataka kujua kama Bwana Jackson Kipng'eno Maswai yuko hapa? Uko! Wewe ndio utafuata Mzee wangu. Wesley Kirui? Wesley Kirui? Bwana Wesley baada ya Mzee utakuwa ni wewe. Halafu Esther Chereng'et utafuata. Halafu Miss. M. Maiwa? M. Maiwa? utafuata wewe halafu Bwana Joseph Chepkwony? Bwana Joseph Chepkwony? ukiwa tayari pia wewe. Rev. William Rotich? Rev. William Rotich? Sawa halafu Julius Yele? Mutafuatana hivyo ndio tufanye kazi iende haraka haraka. Kwa hivyo uendelea utaje jina utoe maoni.

Mr. Philemon Kireni : Asante sana kwa majina ni Philemon Kireni natoka *Chemamul?* Location *Koiolol?* sub-Location. Ni asante sana kwa nafasi ambayo nimepata ile nitoe maoni yangu juu ya maoni ya kutoa Katiba.

Maoni yangu ni kuhusu uchaguzi na uchaguzi ningependa kutoa maoni yangu kwamba...

Com. Abubakar : Ngojea kidogo, nadhani kuna watu wamekuja wame chelewa wa jiandikishe kule na kabla hatuja anza tulisema kwamba kwa sababu tumekitambua hiki kuwa kikao rasmi cha Tume ya kurekebisha Katiba mtu anaye ruhuswa kuzungumza ni mtu anaye toka kwenye meza hii au aliye pewa fursa ya kuzungumza. Ikiwa kuna mtu mwingine anataka kuzungumza waende kando kabisa wazungumze wamalize maneno yao halafu warudi hapa. Hapa pako kama mahakamani, hakuna mtu kuzungumza isipokuwa aliye pewa ruhusa ya kuzungumza. Sijui kama tunaielewana hivyo? Ni sawa? Kwa hivyo tumupe fursa Bwana Philemon Kireni kama wenzake. Bwana Philemon.

Mr. Philemon Kireni : Asante. Nilikuwa nimesema natoa maoni juu ya uchaguzi. Uchaguzi ufanyiwe siku isio wakati wa mwisho wa week. Ifanyiwe siku ambazo ni siku za kazi.

Ya pili ni kuhusu disabled. Kwa disabled ningependa kutoa maoni yangu wapewe employment sawa kama watu wengine. Pili wapewe funds ya kufanya biashara hata wale wako reserve wapatiwe pesa. Ya tatu hapo, ni walemavu pia waruhusiwe wachaguliwe kama viongozi wengine. Nne hapo ningependa pia watoe sheria wasirudishwe kwa magari *[inaudible]* Maoni yangu ya mwisho wapatiwe free medical services na education. Hivyo ndio maoni yangu. Asante sana.

Com. Abubakar : Unaposema unataka walemavu wachaguliwe wawe wana teuliwa, nomination au watengewe vitu vyao, wachaguliwe na walemavu au na watu wenyewe?

Mr. Philemon Kireni : *[inaudible]*

Com. Abubakar : Sawa uende pale ujiandikishe pale tafadhali.

[inaudible]

Com. Abubakar : Mzee Jackson Kipng'eno sasa ni nafasi yako, karibu

Mr. Jackson Kipng'eno : Viongozi wetu kutoka Nairobi watumishi wa Serikali Chemuge, mimi nataka mtu moja kuja hapa kutafsiri ninataka kusema kwa kikalenjin.

Com. Abubakar : Yule Bwana alikuwa akitasfsiri yuko wapi? Mama amekuja.

Mr. Jackson Kipng'eno : Asante. *Maoni ne nyun*

Translator : Maoni yake

Mr. Jackson Kipng'eno : *Eh maoni ne nyun amwae Majimbo*

Translator : Maoni yake ni kuhusu Majimbo.

Mr. Jackson Kipng'eno : *En Majimbo amache ko paikey chi tugul*

Translator : Majimbo yake anataka kila mtu atawale.

Mr. Jackson Kipng'eno : *En koret nyin*

Translator : Katika shamba lake ama kwao.

Mr. Jackson Kipng'eno : No *en Province ne nywan*

Translator : Kwa province yao.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Asi yon ki cheng'e kandoindet i*

Translator : Halafu siku ya kutafuta kiongozi.

Mr. Jackson Kipng'eno : *ke bire kura*

Translator : Wata piga kura.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Si ne ka wosa koik kandoindet ab Kenya ko mugul*

Translator : Na ule atakaye pata ushinde ndio ata kua kiongozi ya hiyo Province.

Mr. Jackson Kipng'eno : Kenya.

Translator : Kenya

[inaudible]

Translator : Viongozi ya kutoka Province ndio ata kua anaongoza Kenya.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ngaliot age*

Translator : Neno lingine.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Kemache sipitalisiek konegitun en sub-locations*

Translator : Anataka mahospitali iwe karibu na sub Location.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Si ko nyor bik kerichek*

Translator : Halafu watu wanapata huduma mzuri na madawa.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Amun ematinwek alak kou Rift Valley ko ..*

Translator : kama kitu ingine kama ya Rift Valley.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ko wo en arawech chu mianwek ne ba iman*

Translator : Kwa hii mwezi malaria ni kubwa sana.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Kemache toretet koyab serikali*

Translator : Anataka usaidizi kutoka Serikali.

Mr. Jackson Kipng'eno : *En somanet amache free Education*

Translator : Masomo anataka ya free education kama ya.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Si konyor bik che terteren*

Translator : Ile wasiojiweza wana weza kupatiwa elimu ya bure.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Agot lagok che matinye sigik ko nyorunen yoton somanet ak ke toret.*

Translator : Hata mayatima wana weza kupata elimu hapo.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ngaliot age kora ko..*

Translator : Neno lingine.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ko kimache foresty korip county council neba district age tugul.*

Translator : Anataka forest ilindwe na County Council ya [inaudible]

Mr. Jackson Kipng'eno : *Amun betos bek.*

Translator : Kwa sababu maji ya chemi chemi imepotea kutokana na wakataji wa miti hovyovy.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ogo ng'ot ko petyo bek*

Translator : Kwa sababu maji ya chemi chemi ikipotea.

Mr. Jackson Kipng'eno : *ugele si kopetyo ko amun kagi yep ketik*

Translator : Itapotea kwa sababu ya ukataji ya miti ile karibu na chemi chemi ya maji.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Konyalu korip district age tugul*

Translator : Lazima District yote alinde forest yake.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Kap chain ireyu..*

Translator : Pahali pa chai ama estate.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Estate ireyu, konyalu korip bik kap district inoton chaik che mi korenywan*

Translator : Pahali pa chai ama estate ni heri watu wa hapo ama District yao ilindwe vizuri.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Si yon kagiib rabisyek ko ba Headquater ...*

Translator : Halafu kama pesa inachukuliwa Headquarter.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ko ye kipyeta kigochi Province age tugul*

Translator : Siku ya kugawanya pesa, kila Province anapata yao.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ak yon kagobwa Province kiyok kobwa District si ko baisien County council.*

Translator : Ikisha fika Province inatumwa mpaka District ili County Council wapate kutumia.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ng'olyot age*

Translator : Neno lingine.

Mr. Jackson Kipng'eno *kimoche toretet en oratinwek ko makitinye en emoni.*

Translator : Wana taka usaidizi kwa barabara, hawana barabara kwao.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ng'olyot age kora*

Translator : Neno lingine tena.

Mr. Jackson Kipng'eno : *ko mi boisieki che toreti kirwogiki chebo kokwotinwek*

Translator : Kuna wazee wasaidizi wa Chiefs wazee wa kijiji.

Mr. Jackson Kipng'eno: *en emotinwek tugul.*

Translator : Kwa nchi yote.

Mr. Jackson Kipng'eno : *Ko monyoru kiy any inne ago toreti serkali. Kimoche musaada kidogo koyob serkali.*

Translator : Hawawezi kupatiwa chochote sasa anataka usaidizi kutoka Serikali.

Com. Abubakar : Sema unataka wafanyiwe nini wazee wa kijiji, walipwe mshahara...

Mr. Jackson Kipng'eno : Walipwe mshahara

Com. Abubakar : Basi hiyo tu.

Mr. Jackson Kipng'eno : Asante. Wana kazi yao wanafanya tu...

Mr. Jackson Kipng'eno : *Chebo education...*

Translator : Umesha sema tayari.

Mr. Jackson Kipng'eno : Okay, okay kuna watoto wale wa hakuna wazazi.

Translator : Mayatima umesema.

Mr. Jackson Kipng'eno : Nimesema...

Translator : Umesema orphans tayari.

Mr. Jackson Kipng'eno : Okay asante. Asante asante. Hakuna mambo ingine. Asante asante

Com. Abubakar : *[inaudible]* Mzee *[inaudible]* Bwana Wesley Kirui? Wesley Kirui? Bwana Wesley Kirui. Njoo tafadhali haraka kila uki jivuta vuta muda unazidi kwenda. Esther Chereng'et ajifanye awe awe tayari. Baada ya Wesley ata kuwa ni yeye. Ndio taja jina uendelee.

Mr. Wesley Kirui : Basi kwa majina naitwa Wesley Kirui, ni asante sana kwa fursa huu nimepata ili nipate kutoa maoni kuhusu Katiba. Yangu kabisa ningependa kutambulisha kusema ya kwamba, sisi vijana tumekosa sana kazi hapa nchini Kenya. Hasa vijana ambao tumesha maliza shule kama sisi. Tuko tu nyumbani bila kazi...

Com. Abubakar : Bwana Wesley hiyo ni stakabadhi tuna jua kwamba kuna ukosefu kwa uajiraji wa vijana, unataka je?

Mr. Wesley Kirui : Basi nataka sasa viongozi, Kenya wote waajiri vijana kama sisi kupata kazi.

Com. Abubakar : Na ikiwa hakuna kazi?

Mr. Wesley Kirui : Basi kama hakuna kazi ufanye juu chini utafutie kazi kama kuelimisha ama upatie yeye sehemu fulani kama kumpuni kama estate ili tupate kazi.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Wesley Kirui : Ya pili tena ningependa kusema ya kwamba free education should be there also. Kwa maana ni...

Com. Abubakar : Kitu kama free education tunaelewa.

Mr. Wesley Kirui : Haya ni asante, so also free treatment.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Wesley Kirui : Haya ndio matatizo yangu ambaye niko nilikuwa nayo kwa asubuhi ya leo, ni asante.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Wesley uende pale ujiandikishe kama umetoa Tume maoni kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Kuna watu wamekuja kuchelewa hawakuelewa muelekeo tulikua tunasema. Tunasema yale yatakayo ingia kwenye Katiba ni mapendekezo. Yale mambo unayotaka ya ingie kwenye Katiba. Ukizungumza kuhusu historia au mambo yanao endelea nchini ya matatizo sisi tunazi... tunaifahamu hayo. Useme tu, kwa elimu nataka hivi. Kwa mambo ya Serikali nataka hivi. Utaje yale unayotaka tu peke yake mapendekezo. Asante sana. Namuomba bi Esther Chereng'et aje atoe maoni yake. Bi Esther ni zamu yako sasa. Karibu. Na mkiona nimemuongezea Mama muda kidogo mujue nafanya ile inaitwa affirmative action. Muacheni mama aseme.

Ms. Esther Chereng'et : Wageni wetu kutoka Nairobi, Chief wetu ma-Chief na viongozi wote serikalini pamoja na wanafunzi. Hamjambo nyote?

Com. Abubakar : Zungumza huko.

Ms. Esther Chereng'et : Maoni yangu mimi na sema asanteni sana kwa ma-officers wetu wale walio kuja hapa siku ya leo na sisi tunaweza kutoa maoni.

Com. Abubakar : Sawa.

Ms. Esther Chereng'et : Maoni yangu nina weza kuwatolea wananchi kuhusu wasichana. Wasichana wasikubaliwe, kila msichana, kila mzazi asikubali msichana wake aolewe akiwa bado mchanga.

Tena wakina mama wajitokeze wakiwa wanataka usaidizi kutoka serikalini musikae tu chini halafu munasema Serikali hapana saidia sisi. Serikali inasaidia kila mtu nimeona mimi mwenyewe.

Wakina mama kwa vikundi vyao, wame wacha vikundi vyao vilale halafu wanasema ati tuna teseka, na hawawezi kujitokeza kwa Serikali ili wasaidiwe. Kwa hivyo hata nimesha sikia kuhusu mambo ya zamani wakati ya wabeberu. Tumeshwa wacha hiyo kwa sababu zamani kuli kuwa ukitaka kupita, ukipita kwa mzungu hata mbwa inaweza kuuwa wewe lakini sisi tuko free siku hizi. Tumepata uhuru ya kutosha.

Com. Abubakar : Mama..

Com. Asiyu : Pendekeza..

Com. Abubakar : Unataka nini. Hii historia tunajua.

Ms. Esther Chereng'et : Tunataka wasichana wasome.

Com. Abubakar : Sawa.

Ms. Esther Chereng'et : Tunataka wasichana wasome kama wanaume.

Com. Abubakar : Sawa.

Ms. Esther Chereng'et : Wakina mama wajitokeze wasaidiwe.

Com. Abubakar : Sawa.

Com. Asiyo : *[inaudible]*

Ms. Esther Chereng'et : Sindio wapatiwe kazi kama wanaume. Kazi ni yote.

Com. Abubakar : Sawa.

Ms. Esther Chereng'et : Walemavu wapatiwe nafasi yao. Haya ni hiyo, asante sana.

Com. Abubakar : Asante sana mama uende pale juu mama ujiandikishe kwa yule Bwana ame vaa shirti la blue pale. Sasa namuita M. Maiwa?

Mr. M. Maiwa : Asante sana Bwana commissioner na Madam Do, na wageni. Kwanza ningetaka kuwasalimu nyingi hamjambo. Commissioner ningetaka kukukaribisha wewe pia na wageni pia na wageni wako. Mimi ndio Chief ya area hii.

Com. Abubakar : Haya Asante sana.

Mr. M. Maiwa : Karibu sana. Mimi niko na vitu tatu tu. Ningetaka Chief Act irudishwe vile ili kuwa. Nguvu ya Chief ibaki kwa sababu kazi ya wananchi haiwezi kuendelea bila Chief. Kwa hivyo powers ya Chief ibaki vile iko. Hiyo ndio nasema.

Com. Abubakar : Number one.

Mr. M. Maiwa : Number one. Ya pili wafungwa wale ambo wame wanastakiwa wamefanya makosa ndogo ndogo, ningomba kwa sababu kwa kifungu hapo jela wengi wanafariki. Hii makosa ndogo ndogo, irudishwe apewe Chief, hawa maabusu ambaye wamefungwa aletwe ikae kwa Ofisi ya Chief na afanya kazi ya wananchi.

Com. Abubakar : *[inaudible]* watu wanaofanya makosa madogo madogo wafungwe kifungu cha inje. Warudi kwao wapewe kazi za kufanya na kusaidia maendeleo, sijui pengine haifanyiki inavyo takikana. Lakini hivyo ndio sheria iko sasa.

Mr. M. Maiwa : Nimesema haifanyiki.

Com. Abubakar : Sawa.

Mr. M. Maiwa : Mimi sijaona kwa ofisi yangu.

Com. Abubakar : Okay sawa

Mr. M. Maiwa : Ya tatu kazi ya Serikali ya Magistrates na Judges pia imekuwa ngumu. Na tuko na ma Do's kwa kila Division. Na mbeleni walikuwa pia wanapewa nguvu ya ku fanya cases kwa ofisi zao.

Com. Abubakar : *[inaudible]*

Mr. M. Maiwa : Akae tu kama Magistrate ndio irahisishwe kazi ya Judges ambaye iko kwa District na afanye pia cases ile ndogo ndogo. Hawa wafungwa tena ibaki hapa badala ya kupeleka ifungwe huko prison. Hiyo ndio itasaidia wananchi.

Halafu hii kosa kubwa kubwa murder nini watu wafungwe sababu atakuja kuuwa wewe.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. M. Maiwa : Asante

Com. Abubakar : Asante sana

Com. Asiyu : Niko na swali

Com. Abubakar : Asante sana Chief subiri kidogo...

Com. Asiyu : Nataka kukuuliza hivi watu wengi wametueleza kule ambako tumekwenda kwamba kwanza wangependa ma-Chief wachaguliwe na wananchi, wengine pia wame tuambia wanataka ma-Chief wawe-transferable kwa District yao kwa maana wengine wanasema ukionelewa na, Chief akikuonea mpaka siku ile atakufa ama atawacha kazi ndio hiyo kuonea inakwisha au kama baba ya Chief aligombana na baba yako kwa shamba hiyo Chief anakushikilia tu mpaka siku ile anakufa ndio unapata nafasi, lakini akipewa transfer kama vile sisi husema watu wengine wanapewa mtu anapata nafuu. Wewe sasa utueleze kama Chief unapendelea ma-Chief wachaguliwe na wananchi au waandikwe tu na Serikali lakini wawe transferable au unataka wakae vile walivyo kwa wakati huu.

Mr. M. Maiwa : Hiyo nime kataa.

Com. Asiyu : Ni ipi ume kataa

Mr. M. Maiwa : Chief hawezi kuchaguliwa na wananchi, ana chaguliwa na Serikali

Com. Asiyu : Na

Mr. M. Maiwa : Kwa sababu wakichaguliwa na wananchi wata chagua ile mtu mbaya kabisa, labda ile mtu mlevi, na yule hata weza kuongoza Location.

Com. Asiyu : Na habari ya transfer.

Mr. M. Maiwa : Transfer hiyo haiwezekani kwa sababu mimi ndio, ni kama nyumbani tu ni Mzee ya kijiji.

Com. Asiyu : Okay sawa sawa nime shika.

Mr. M. Maiwa : Na kuni letea sasa mtu mwingine kutoka huko ana jua watu yangu.

Com. Asiyu : Sawa sawa.

Mr. M. Maiwa : Hiyo nime kataa

Com. Abubakar : Haya asante sana Chief, asante sana uende pale Bwana Chief.

Mr. M. Maiwa : Asante.

Com. Abubakar : Ujiandikishe kwamba umetoa maoni kwenye Tume ya kurekebisha Katiba. Asante Chief. Sasa namuita Bwana Joseph.. Huyu alikuwa ni Chief Joseph Chepkwony, no, huyu alikuwa ni Bwana Chief Maiwa sasa namuita Bwana Chief Joseph Chepkwony? Karibu

Mr. Joseph Chepkwony : Do, wageni na wananchi hamjambo? Jina yangu ni Joseph Chepkwony, mimi ni Chief kutoka *Kiptome*? Yangu ni machache kabisa. Okay. Yangu ni machache kabisa, ya kwanza ni kuhusu powers of the Chief irudishwe kama zamani kwa sababu wakati huu tuko na wengi na wengi ni wakosaji.

Ya pili ni kuhusu succession, mambo ya property of the Parents, ipatiwe watoto iwe equally.

Na ikiwa wasichana wameolewa, ikiwa kama wameolewa ita tegemea kama mzazi ame andika urithi yake.

Ya tatu ni kuhusu mambo ya President. Hiyo limit iwe limit ya two terms, ingefanyika kama ile ya British ichaguliwe kama watu wanapenda. Ikiwa watu wanapenda iendeleo.

Nafikiri hiyo imetosha.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Chief uende pale ujiandikishe umetoa maoni kwenye Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya. Rev. William Rotich? Karibu Reverend.

Rev. William Rotich : Yangu tu ni machache. Jina langu ni Reverend William Rotich kutoka kanisa la Apfk Free Pentecostals Fellowship in Kenya. Maoni yangu tu ni juu ya uhuru ya kuabudu. Hata ingawa kuna hii mambo ya kusema ya kwamba uhuru ya kuabudu. Kuna wengine ambao wana abudu sheitani na hiyo ni uhuru ya kuabudu. Inge faa tu iandikwe ya kwamba uhuru ya kuabudu Mungu na iwe hivyo tu. Kuliko kuandika tu ya kwamba uhuru ya kuabudu, hata watu wanaweza kuabudu watu.

Sisi kama kanisa tena lazima tuwe na Minister wetu wa religious Minister kuliko tuchanganishwe na watu wengine kwa sababu sisi ni wengi katika Kenya.

Tena kuna Duty free ya saa ingine tunaye Donors ambao wana weza kutusaidia katika kanisa. Lakini inaonekana kama kuna, inge andikwa tu ya kwamba free duty kwa kila kanisa kuliko hii mambo ya kusema ya kwamba kanisa hii ipate na hii ipate, na zingine hawana hii free duty kutoka mahali ingine.

Nafikiri hiyo machache ambaye ninaye. Thank you.

Com. Abubakar : Asante sana Reverend. Ujiandikishe pale ume toa maoni kwenye Tume ya kurekebisha Katiba. Julius Siele? Bwana Julius Siele? Bwana Julius Siele mara ya pili. Nilikuwa nasema nitaita mtu mara mbili. Hayuko. Munakumbuka tulipoanza nilisema kwamba tuna kama Tume tuna haki ya kumpa mtu fursa ikiwa kuna sababu za kutosha. Sasa ningependa kumpa Councillor Richard Samoe fursa azungumze halafu aende kushughulikia mambo mengine muhimu. Councillor.

Mr. Richard Samoe : Mimi ni Councillor Richard Samoe naibu wa mwenye kiti baraza la Kipsigis County Council. Mapendekezo langu ni kwamba ningependa Serikali kuu wapeane uwezo mabaraza yote ili wawe na nguvu ya kuweza kuendesha mambo yao.

Na pia ningependa pia baraza wajisimamie haswa kama mashamba makuu ya majani chai ambao inaendeshwa na watu ambao inatoka mbali. Na wenyeji wana taabika na hakuna usaidizi hata kidogo kutoka upande hiyo. Pia...

Com. Abubakar : Kwa hivyo ungetaka aje kabla? Yaani kama mashamba kama hayo Council iwe na haki ya kutoza kodi kodi isaidie wananchi.

Mr. Richard Samoe : Kabisa. Na pia ningependa pia nguvu ipewe Councillor kwa sababu unaweza kuta Diwani anaweza kuwakilisha area ambao wako na Chief wawili na manaibu wanne. Na mshahara hiyo Councillor anapata ni kidogo sana na hawezi kuwezesha kuendesha kazi vile inavyo takikana.

Com. Abubakar : Kwa hivyo unataka je [*inaudible*].

Mr. Richard Samoe : Inge faa Councillor ipewe nguvu zaidi. Mimi nafikiri ni hayo machache.

Com. Abubakar : Asante sana Councillor, Vice-Chairman tafadhali uende pale utoe sign- kwamba umetoa maoni kwetu. Josiah Sang? Josiah Sang? Karibu Bwana

Mr. Josiah Sang : Asante sana Commissioners, Madam Do ma-Chiefs na wananchi. Yangu tu ni machache ningependa kutoa maoni kuhusu marekebisho ya sheria. Kwa majina mimi ni Josiah Sang Chief kutoka *Kiboinet*? Location katika tarafa ya Sikowet. Niko na mambo mawili matatu hivi.

Kwanza kulingana na Defence na National Security iwe jukumu la Rais, vile ilivyo kwa Katiba.

Kuhusu political parties ipunguzwe iwe mbili.

Structure na vile Serikali inataka ikuwe ningependekeza Federal system Serikali ya Majimbo. Yaani tuwe na Federal

Government na ile ingine Distinct Regional Government.

Halafu ya mne katika basic rights kuhusu social and economic na cultural iwe iandikwe mzuri kua sheria.

Kama ni shelter watu wa angaliwe vizuri tujue tuna shelter ya aina gani. Kama ni chakula, food security iwe ya kwanza. Kwa sababu iko na sehemu zingine ambao hakuna vyakula.

N kuhusu education. Tuwe na free education ya Primary level na iwe compulsory. Ningependekeza hivyo up to Primary level.

Na ya Civil Rights watu wafundishwe Civil Education, yaani wajue Rights yao iwe ni jukumu la kuendelea.

Hiyo tu kwa wakati.

Ya mwisho ningependelea kwamba Chiefs Act irudishwe kama ilivyo kuwa halafu watu wana hudumiwa vizuri. Asanteni.

Com. Asiyo : Niko na swali moja tu *[inaudible]*

Mr. Josiah Sang : Ningependekeza...

Com. Asiyo : *[inaudible]*

Mr. Josiah Sang : Ningependekeza ya kwamba katika federal system ya Government vile mume kuwa split ya Executive na Legislature authority na Distinct Regional tuwe Governor ya Regional, na tuwe na Prime Minister.

[inaudible]

Com. Abubakar : Sasa mama akiwa tayari aniambie tu. Hata sasa hivi mimi naweza kumpa fursa mama aseme. Haya uko tayari. Mama unaweza kukaa tu hapo. Hakuna wasiwasi.

Mama Sophia arap Too : *Ochomege tugul is. Okotok tugul ale ochimege?*

Translator : Nyingi nyote hamjambo.

Mama Sophia arap Too : *Awekyini kongoi Jehovah amun ripset ne kokoribon kot anyoru asistab raini.*

Translator : Namrudishia mwenyezi Mungu asante kwa vile amenilinda mpaka kwa siku ya leo.

Mama Sophia arap Too : *Ko noton boiboiyenyun.*

Translator : Na hiyo ni furaha yangu.

Com. Abubakar : Mama sema jina yako.

Mama Sophia arap Too : *Kainenyun ko Sophia nebo arap Too.*

Translator : Jina lake ni Sophia bibi wa Too.

Mama Sophia arap Too : *Ko en tuiyoni ko komoche kinetan korok kit ne bo amun ang'alale nee komokuitosi.*

Translator : Na katika mkutano hii anataka afunzwe kwanza aelezwe vile inaendelea kwa sababu yeye amefika sasa.

Com. Abubakar : Sasa mama [*inaudible*]

Translator : (*Inaudible*)

Mama Sophia arap Too : *Ko en ng'alekyuk*

Translator : Maneno yake.

Mama Sophia arap Too : *Uon koto ang'alal mising akobo nga'leKab kwonyik ak monung'otoik.*

Translator : Angependa kusema sana juu ya hali ya akina mama na wanaume zao.

Mama Sophia arap Too : *Amun mwowon Bible, tomwoe chemiBible, kole amun ng'olyot ne kiakas kele en nga' tutichu kotyagat chi tuguk koyai kasit, chi tugul, ityagat kabisa.*

Translator : Kwa vile anategemea Bibilia na vile amesikia ya kwamba kina mama ama kila mtu ako na uhuru

Mama Sophia arap Too : *Kou ye kichob Jehovah.*

Translator : Kwa vile Mungu alimuumba

Mama Sophia arap Too : *Agas en yon Kokeny*

Translator : Na tena akasikia ya kwamba.

Mama Sophia arap Too : *ko uhuru nebo chepyosok ko uhuru koyai kasit lakini ma uhuru en konyin.*

Translator : Na vile anavyo fahamu ya kuwa, uhuru ya akina mama ni uhuru ya kufanya kazi lakini si uhuru ya kuwa na nguvu katika nyumba yake.

Mama Sophia arap Too : *Si amwa kou noton kwokose en redio kirwoget ne kirwokyin kwondo ne kokimuti en olin ak manung 'otiot ne kikobar.*

Translator : Anavyo sema hivyo alisikia katika radio walikuwa wakitangaza mama moja ambaye alikuwa ame, mwenye aliua Bwana yake.

Mama Sophia arap Too : *Ko noton en Kipsigis, en bikap Kalenjin*

Translator : Na kwa Kipsigis, watu wa Kalenjin.

Mama Sophia arap Too : *ko kimako bouge kwondo kou ng'otutichu moe konde serkalit koboige kwondo asi koget manung 'otoik.*

Translator : Na katika desturi ya kikalenjin niya kwamba mwanamke hangepewa uhuru ya kukuwa na nguvu ili aweze kua Bwana yake.

Mama Sophia arap Too : *En ng'alekab Jehovah ko kiyai, amache en yon, ogonon bible o.*

Translator : Na kwa maneno ya Mungu inatufundisha ya kwa katika Bibilia

Mama Sophia arap Too : *Amache asoman ng'alek amun Jehovah ko nekiyoech.*

Translator : Sasa yeye atasema maneno ambaye iko kwa Bibilia kwa sababu Mungu alituumba.

Mama Sophia arap Too : *Mi ng'alek che tinye uhuru akomi ng'alek che matinye uhuru.*

Translator : Kuna maneno ambaye iko na uhuru na iko na kuna yenye haina uhuru.

Mama Sophia arap Too : *Ko amun asikoyait emet kot ko ngunon komi atebosiek che u chu ko amun kikobut lagok ng'atutik, kobut sigik ng'atutik.*

Translator : Na vile tunaona mambo yame elekea imeharibika ni kwa sababu ya wanawake kutotii sheria ya Bibilia.

Mama Sophia arap Too : *Ko amun Jehovah ne kiyoech komoche kisib kalyet. Abaibai en Kenya amun kalyet.*

Translator : Mungu aliye tuumba anataka yakuwa tukaye na amani.

Com. Abubakar : Muambie Mama kama nimelewa kama vile alivyo sema yeye hataki wanawake wawe na uhuru kushinda yule ulio tolewa na Bibilia.

Mama Sophia arap Too : *Ee. Soman tounet o.*

Translator : Na vile amesema ya kuwa, amekubaliana na wewe lakini bado anataka Bibilia isomwe.

Com. Abubakar : Soma

Mama Sophia arap Too : *Taunet somok. Ngoro nebo Kipsoili any o. Soman any, soman chitab Kipsoili, soman any.*

Translator : Sasa anataka tusome katika kiswahili.

Com. Abubakar : Usume mara moja.

Translator : Nitasoma mara moja

Com. Abubakar : *[inaudible]*

Mama Sophia arap Too : *Taunet somok.*

Translator : Tutasoma kutoka kitabu cha mwanzo. [Genesis]

Mama Sophia arap Too : *Ak kaitet taman ak aeng'*

Translator : Mlango ya tatu.

Mama Sophia arap Too : *kot koit taman ak sogol.*

Translator : Tuanzie kumi na mbili mpaka kumi na tisa.

Mama Sophia arap Too : *Si ogas tuguk che mochomdoi Jehovah.*

Translator : Sasa inasema ya kwamba, “Bwana Mungu aka muambia mwanamke, nini hili ulilolifanya mwanamke akasema nyoka alinidanganya, nikala. Bwana Mungu akamwambia nyoka, kwa sababu umeyafanya haya umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko haya, haya walio wote walioko mwituni kwa tumbo utakwenda na mavumbi utakula. Siku zote za maisha yako nami nitaweka adui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake. Huyo utaku ponda kichwa na wewe utamponda kisigino na akamuambia mwanamke hakika nitakuzidishia uchungu wangu kwa kuzaa kwako, kwa uchungu utazaa watoto na tamaa yako ita kuwa kwa mumeo naye ataku, atakutawala, akamuambia Adamu kwa kuwa umei sikiliza sauti ya mwanamke wako, ukala matunda ya mti ambayo nilikuagiza nikisema usiyale, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako kwa uchungu uta kula mazao yako siku zote za maisha yako. Michangamo na miba itaku zalia na nawe utakula mboga za kundeni kwa jasho la uso wako utakula chakula hata utakaporudia ardhi ambayo katika hiyo uli tawalia, kwa maana huu mavumbi wewe nawe mavumbini utarudi.

Mama Sophia arap Too : *Ko ng'olyot nemi yon ko ne kimwoe Jehovah kwondo kolenji inyoli monung'otiot.*

Translator : Maneno yale ambayo tumesoma Mungu aliambia mwanamke utaangalia Bwana yako

Com. Abubakar : Asante ambia mama asante sana.

Translator : Asante

Mama Sophia arap Too : Asante

Com. Abubakar : Ndirangu uje na kitabu mama assign hapa hapa tu. Hii kitabu kijana ana kuja nayo usign. Asante sana

Mama. Sasa namuita Bwana Samuel Ruto? Bwana Samuel Ruto? Karibu Bwana. Oluoch hii microphone u-i-adjust tafadhali

Mr. Samuel Ruto : Kwa majina mimi ni Samuel Ruto, Senior Assistant Chief kutoka *Kebeleti*? Nina machache ambao ninataka kusema. Juu ya elimu: Elimu tunataka iwe free na iwe free kwa watu wote, kwa wanafunzi wote, ya Primary, Secondary na walemavu, na wale ambao wanajiweza.

Naendelea tena na mambo ya inheritance: Mambo ya urithi wengine wasi baguliwe tuwache hii ya custom watoto wote wawe beneficiaries ya mali ya nyumbani.

Environment: Tumeona siku hizi watu wana destroy forest...

[inaudible]

Mr. Samuel Ruto : Hiyo iwekwe tena uchungaji kutoka kwa watu wote hata kwa village, village elders, wawe involved na kila mtu hata farmers, kwa sababu imefika wakati ambao tumekosa mvua halafu tuta complain.

Com. Abubakar : Sawa, sawa

Mr. Samuel Ruto : Ingine ni equal services for all the Kenyans: Wale wanaajiriwa wawe sawa waume kwa wake.

Kuna tena siku hizi orphans kutoka wale victims of Aids wa angaliwe tena kwa sababu hiyo ni tatizo la taifa na tuwe tukitowa reports kwa wale ambao wame adhiriwa ili Serikali iweze kutambua na kusaidia.

Equal employment: nilikuwa nimesema.

Asante sana. Ni hayo machache.

Com. Abubakar : Asante sana Mzee unipe hiyo microphone tafadhali.

Hallo, hallo, hallo, hallo...

Com. Abubakar : Haya namuita sasa Bwana Charles Kilel? Bwana Charles Kilel? Tulikubaliana namuita mtu mara mbili hayuko naenda kwa Jane Kipkoech Korrir? Bwana Kilel? Wewe uko? Kwa nini unachukuwa muda mrefu kuja namna hiyo. Hebu subiri hapo nitaje watu majina yao wajue nafasi zao za kuja. Baada ya Bwana Charles Kilel, atakuja Jane Kipkoech Korrir, atafuatiwa na Fred Ng'eno, atafuatiwa na Benjamin Mutai, na atafuatiwa na Rael Mirgor. Hao wakae karibu na chonjo

kabisa niki muita mtu anakuja kabla sija mkata.

Mr. Charles Kilel : Yangu ni machache ningependa kutoa maoni yangu kuhusu *[inaudible]* kwa majina yangu naitwa Charles Kilel. Yangu ni machache ningependa kutoa maoni yangu kuhusu Serikali ya majimbo, ningependa Serikali ya majimbo.

Kuhusu Chiefs Act ibaki vile ilivyo sasa na wananchi wachague ma-Chiefs.

Jambo lingine kuhusu mashamba, tumeona kuna watu wengine wako na mashamba makubwa na wengine hawana hata kabisa. Sasa tungependa Serikali watoe hata nini ama sheria, yaani pahali hawa watu wenye wako na mashamba makubwa wagawanyie wenye hawana kabisa.

Halafu lingine ni free education. Na lingine sasa ni free education free health services and accessibility Serikali ya ingie kabisa mpaka *machinani*?

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Charles Kilel.

Speaker[s] : *[inaudible]* Hallo

Com. Abubakar : Yeah! Zote za fanya sasa.

Speaker[s] : Wacha tutumie hii basi.

Com. Abubakar : Unataka tutumie pale hii.

Speaker[s] : Hallo, hallo, hallo

Com. Abubakar : Hii ndio ina sauti kubwa. Namuita Jane Kipkoech? Dada karibu. Kwa wale watu wanaofika sasa kuna yule Binti pale anaandikisha watu majina ukiwa unataka kuzungumza uende pale ujiandikishe.

Ms. Jane Kipkoech : Maoni yangu ni kuhusu Katiba ninge furahiya kuna wamama waetima wenye wame wachwa na wazee wao na hawana makao mahali wenye wanakaa, kwa hivyo hata kusomesha watoto wao ni shida sana maana hana usaidizi yeyote yenye anaweza kusaidiwa. Sasa ningepomba Serikali ione wale wamama wenye hawana wazee yao wapate usaidizi.

Ni hayo yenye ninge, nilikuwa nayo sikua na mengi.

Na kuna wasichana pia wenye wamezaa nyumbani inatakikana wapate usaidizi maana hata hawana makao na wana watoto hata kusomesha wale watoto yao wako na shida ya kuweza kusomesha watoto na unakuta watoto wana andikwa na watoto wanapata matatizo. Maana watoto hawawezi kulelewa vile unaweza kulea mtoto yako wewe mama mwenyewe. Hapa ningeomba pia wa angaliwe pia hayo wasichana wasaidiwe.

Com. Abubakar : Asante sana bi Jane, tafadhali uende pale juu ujiandikishe. Namuita sasa Fred Ng'eno? Bwana Ng'eno? Benjamin Mutai na Rael Mirgor wakae tayari tayari karibu.

Mr. Fred Ng'eno : Yangu [*inaudible*] jina langu ni Fred Ng'eno.

Com. Abubakar : Endelea.

Mr. Fred Ng'eno : Yangu ni machache.

Com. Abubakar : Songea Karibu, Songea karibu.

Mr. Fred Ng'eno : Yangu ni machache.

Com. Abubakar : Sawa.

Mr. Fred Ng'eno : Kama ningekuwa na uwezo tungepatiwa free education.

Com. Abubakar : Sawa.

Mr. Fred Ng'eno : Ile tumalize ujinga katika hii Kenya yetu

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Fred Ng'eno : Tupatiwe tena free treatment.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Fred Ng'eno : Ile kitu mimi na onelea tena ni mambo ya corruption, corruption Serikali ange-select commission

ambaye anaweza kusimamia mambo ya corruption lakini sio Kenya Police and Anti-Corruption Unit.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Fred Ng'eno : Nafikiri ni hiyo tu.

Com. Abubakar : Asante sana Bwana Ng'eno uende ujiandikishe pale. Bwana Benjamin Mutai.

Mr. Benjamin Mutai : Asante sana ma-Commissioners mimi ni Benjamin Mutai Diwani kutoka upande wa Kiptere. Ningependa kutoa pendekezo kwa ma-Commissioners wa sheria na la kwanza, ningependa kutaja mambo husu soko huru ama liberalization ningependa kusema liberalization inge kuwa kwa kiasi fulani kwa yale vitu ambaye hayako katika upande wetu.

Na la pili ningependa tena kusema sheria hainge bagua watu wengine, kwa kuwa wakati huu uwa wana ubaguzi wakati mwingine katika sehemu za masomo. Facilities uwa upande mwingine nazidi upande mwingine wengine wakati wengine hawana facilities za kutosha, hata wakati wa kuandikisha mashule, upande mwingine wanahitajika kuwa na acre tano na wengine wanasomea hata juu ya gorofa, na hawana mashamba ya ku kimbilia kimbilia.

Na la pili ama la kumalizia, ningependa kusema makanisa wangepewa uhuru wa kuabudu na vile mwenzangu alikuwa amesema uhuru kuabudu Mungu sio kuabudu Sheitani.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Benjamin Mutai : Naweza kusema tu ni hayo machache tu.

Com. Abubakar : Asante sana Councillor tafadhali ujiandikishe pale kwamba umetoa maoni na hiyo memorandum utuwachie. Asante Sana. Rael Mirgor? Rael Mirgor? Rael Mirgor mara ya mwisho. Sasa nitaita majina, Fanice Chepkwony? Dada kiasi anakuja nataka Joyce Mutai, Lilly Lang'at, Samuel Koech, na Bernard Cheruiyot wajitayarishe. Ngoja ngoja ngoja dada. Joyce Mutai yuko? Uko wapi? Uko hapa. Lilly Lang'at njoo huku dada ukae hapa karibu na hichi kiti cha hapo. Samuel Koech? Samuel Koech? Samuel Koech hayuko. Bernard, Doctor Rotich Joseph ukae hapa karibu tafadhali, Bernard Cheruiyot? Bernard Cheruiyot? Hayuko? Bernard hayuko. Retired Chief Ezekiel Tanui? Uko? Uko karibu, asante sana. Dada endelea.

Ms. Fanice Chepkwony : Okay

Com. Abubakar : Songea karibu na mic kabisa uinue kidogo, inue juu kidogo.

Ms. Fanice Chepkwony : Ya kwanza kabisa *[inaudible]* jina langu ni Fanice Chepkwony...

Com. Abubakar : Fanice hiyo mic inue kidogo hivi. Halafu usongelee karibu hivi, songelea karibu hivi.

Ms. Fanice Chepkwony : Jina langu ni Fanice Chepkwony kutoka Kikowet Maendeleo Women's Group. Ningetaka ya kwanza kabisa wasichana wasome kama wavulana.

Ya pili circumcision ikome kwa wasichana kabisa.

Ya tatu wasichana wale wamepata watoto nyumbani wapate mali tena ya...

Ms. Joyce Mutai : ...Kabla sija endelea mbele ningependa kuwa salimu nyote katika jina la Yesu hamjambo? Kwa majina naitwa bi Joyce Mutai na ningependa kuongea... *[inaudible]* juu ya akina mama. Hapa nimeonelea ya kwamba wamama wanapaswa kulindwa hasa kwa maendeleo yao na inafaa sana kwa akina mama wawe na akili ya kutosha ili waweze kuchunga nyumba zao.

Ningependa tena kusema ya kuwa tohara kwa wasichana iondolewe kabisa iwekwe sheria katika Kenya yetu ya kwamba mwenye anaweza kufanya wasichana wa tairishwe hiyo sheria ikaziwe sana hata wapate hata kushikwa wafungiwe.

Na mambo ya masomo kwa wasichana ningependa kutia nguvu sana kwa sababu vile tunaona katika hapa kwetu Kipsigis mambo ya wasichana sana sio, haina nguvu sana kwa msichana kusomeshwa lakini ningependa kusema ya kuwa mutuwekee katika sheria ya kwamba masomo kwa wasichana iwekwe nguvu kama ya mvulana. Nafasi ya kazi ikipatikana nao pia wawekewe katika mstari ya mbele kama wanaume ili wapate kufanya kazi kwa vile tuna jua ya kuwa wote ni watu.

Hekima kwa wanawake nasema ya kwamba afadhali ama vile ninaonelea tungependa sana wanaume waheshimu wanawake ili wanawake wawe na upendo katika nyumba zao ili mambo yote ya kuwe mazuri.

Sheria ya kutunza mayatima tena ningependa kukaza sana zaidi ili tu weke katika sheria ya kwamba mayatima yatunzwe vilivyo. Mayatima wasiwekewe katika line ingine ambaye isio faa ama wateswe ama wawekewe kwa mambo mengine.

Mambo ya viziwi kwa jumla ningependa kukaza sana tuone vile tutalinda hawa wawekewe katika mstari moja sawa na watuwengine.

Com. Abubakar : Sawa

Ms. Joyce Mutai : Wasichana wasio olewa ningependa sana kukazia kwa vile tunaona katika kijiji yetu wasichana wasio olewa wako kwa wingi. Na ningependa kukazia hio sheria ya kwamba, Serikali iangalie hao wasichana, watunzwe ili wapate nguvu nao pia hapo mbeleni wanaweza kupata kazi, ama wanaweza funzwa kazi ya mikono ama wafundishwe mambo mengi.

Com. Abubakar : Sawa

Ms. Joyce Mutai : Wazee wakongwe. Vile ninaonelea wazee wakongwe afadhali wa wekwe pamoja kwa sababu wengine kufaa kabla kufika wakati wao na vile ninaonelea vile ninaona wamama wakongwe ana wazee wawekewe pamoja watunzwe ili wawe na nguvu na wapate kukaa miaka nyingi.

Com. Abubakar : Unataka wajengewe nyumba peke yao?

Ms. Joyce Mutai : Wajengewe kama shule...

Com. Abubakar : Au wapewe allowance waangaliwe kule wako?

Ms. Joyce Mutai : Serikali iwatunze. Mambo ya wasichana wenye wameenda pale town ama niseme tu Malaya. Afadhali tuweke sheria ya kwamba wasichana wote wakomeshwe kwenda huko town na wafundishwe wafanye kazi fulani ili wapate, ili tupate hii mambo ya Ukimwi ikome.

Asante sana

Com. Abubakar : Asante sana dada uende pale juu ujiandikishe kwenye yule Bwana mwenye shirt ya blue. Asante sana. Lilly Lang'at. Utaje jina na usongee karibu kabisa na mic, karibu kabisa.

Ms. Lilly Lang'at : Kwa majina ni Lilly Lang'at.

Com. Abubakar : Songea karibu

Ms. Lilly Lang'at : Kwa majina ni Lilly Lang'at kutoka Sikowet Women's Group. Kwa machache nataka kusema kidogo tu yangu ni kusaidia wa group finance ili tuende kwa vijiji tu hubiri maneno ya Aids control na kusaidia watu wale iko kwa nyumbani hatoki kusikia maneno kwa hapa kwa makutano. Sasa tunaomba mikopo kwa wa kina wa mama wa Sikowet ili tutembe wafundishe wengine wako nyumbani.

Com. Abubakar : Sawa

Ms. Lilly Lang'at : Ya pili tunaomba wale wamama wame olewa kwa mtu moja asifukuzwe tena, kufukuzia mwengine kwa maana Aids Control imetembea sana.

Ya tatu ni leaders. Tume, juzi tume sikia kwa Baba yetu Moi alisema anataka wachia vijana kiti yake. Basi tunaomba kwa Katiba yetu akina mama kama iko mtu moja nana pambana na kama ni Mzee anataka kiti ya President wetu awachwe Mzee wetu aendelee halafu uchunge sisi wakina mama. Kitu tunaomba sana.

Kitu ya mwisho. Tunaomba wako na wazee wengi na wakina wamama wame wachwa na vijana wao kwa maana watu wadogo wame weza kuenda kwa Ukimwi sasa apewe mkopo asaidie akina wazee an wakina wamama kwa Serikali yetu ya mtukufu Rais ili apate mkopo kwa ma nyumbani kwa maana Serikali hapana weza kuchunga sana kama ile mkopo amepeana kwa nyumbani.

Asante sana.

Com. Abubakar : Asante sana bi Lilly uende pale juu ujiandikishe. Sasa namuita Bwana Rotich Joseph.

Mr. Joseph Kibii Rotich : First I want to address the issue of land.

Com. Abubakar : Anza na jina lako.

Mr. Joseph Kibii Rotich : Joseph Kibii Rotich. The issue of land has been a thorny issue for many years and we have issues like squatters, we have issues like...

Com. Abubakar : *[inaudible]* kabala huja kuja nilikuwa na ambia watu historia hadithi hatutaki. Hakuna mkenya hajui habari ya squatters, tuaambie tuta-solve namnagani, what are your proposals?

Mr. Joseph Kibii Rotich : What we want to do...

Speaker[s] : *Nimwa en Kipsoili o, si kegas.*

Mr. Joseph Kibii Rotich : We have the squatters as I have said...

Com. Abubakar : Mzee mama anataka useme kiswahili

Mr. Joseph Kibii Rotich : The issue of land which was leased to the foreigners, which was leased by somebody we don't know, we would wish to have the land being addressed by the community. We would like also to see those people who were displaced compensated.

Com. Abubakar : Sawa

Mr. Joseph Kibii Rotich : And on the same issue the landless be given land.

Second agriculture the issue liberalization as we now has killed the agricultural sector. You know that one. What we are against is the importation of sugar for example, the importation of milk for example, the importation of all those things...

Com. Abubakar : So what you want is not to allow the importation of agricultural...

Mr. Joseph Kibii Rotich : Yes to kill our own agriculture.

Let us go to health: We want the ministry of health to provide free medical services because the sharing be revoked.

Education: We would want to see free education from form one to form four. Following that the issue of, free education free supplying of school equipment as it used to be. We used to have Kenya School Equipment Scheme to be revived.

Employment: As far as employment is concerned every Kenyan should be guaranteed by the Constitution of employment.

Com. Abubakar : *[inaudible]*

Mr. Joseph Kibii Rotich : In the absence of employment they should provide what you call social security...

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Joseph Kibii Rotich : Fund, and the issue of what we call experience before one is employed is illegal and ill-motivated.

The powers of the President should be drastically reduced. The power to elect the Electoral Commission out, the power to appoint the Chief Justice out, and be taken to the Parliament because that is where we believe our eyes lie.

We have also the issue of parties we would wish to have three parties at least.

Mp's be at least graduates and people who are morally right.

Councillors be at least form four.

Nominated or nomination should be done by the public or the community where those people are expected not by a few people.

Majimbo system of Government or federal system is what we want, with the highest elected office of the Prime Minister who will hold executive powers than anybody else. The President being a ceremonial President.

Ombudsman, you understand that, office be created at the District level where they will be listening to the cries and what and what of the people.

As far as the elected posts are concerned like that one of an Mp, I'm sorry for referring you back, in the Constitution there is that clause that says if the Mp fails to attend Parliament for 8 consecutive days he should cease to become. We said if an Mp fails to attend his people for at least a maximum of 3 months should cease to become an Mp.

I tend to think that also the issue of water the issue of forest, the issue of game reserves be vested upon the public and the Government.

For these few remarks I say thanks for now.

Com. Abubakar : Asante sana Daktari unaona ulipoanza kua focused siku ku interrupt. Asante sana uende pale u-sign kwamba ume toa maoni kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Asante sana Daktari. Retired Chief Ezekiel Tanui. Karibu mzee

Mr. Ezekiel Tanui : Viongozi wako hapa leo sababu ya sheria yetu ya kurekebisha. Jina yangu ni Ezekiel [inaudible] Yes, jina yangu ni Ezekiel Tanui from Sikowet Division. Mimi ningetaka kusema maneno maoni yangu ni kidogo kuhusu wazee na wakina mama. Wale wamesha fika miaka hamsini na kwenda mbele mimi nataka kuomba Serikali ukumbuke badaye wapatiwe cess. Cess sababu wakati hiyo kuna shamba, watu na kwisha kuwa wengi ile mtu ulikuwa na fanya kazi kwa nchi mpaka nchi imekuwa tajiri wazee wanatakiwa kupewa chakula siku hiyo kina mama na wazee. Ya miaka hamsini na kwenda mbele. [inaudible].

Ya pili, tunataka sheria ya kumpa nguvu watu hapana kaa bila kazi. Kwa sababu kama watu na kwisha kuwa wengi na hakuna

kazi ya kufanya na ongeza taabu.

Ya tatu, mimi kuna shamba kidogo kidogo iko Title Deed mbona Serikali hapana pea sisi stima halafu tupate kulipia pesa kidogo kidogo mpaka deni na kwisha.

Ya nne, wasichana, wasichana wetu na wasichana wetu nataka kutafutia hawa sheria ya kuwacha mtindo ya kutembea ovyo ovyo, na kuongeza marifa mbaya mbaya bila, mpaka nchi haiku kuwa ha *hekima*?

Na komea hapo.

Com. Abubakar : Asante sana Mzee uende pale Mzee ujiandikishe, asante sana. Sasa namuita Joseph Sigilai? Bwana Joseph Sigilai? Halafu wale wengine, Eric Kerich? yuko hapa? Eric? Eric Kerich? Narudia mara ya mwisho, Eric Kerich? Wewe ni Joseph sio? Wewe ni Eric? Eric subiri pale, nimemuita Joseph Sigilai? Joseph Sigilai? Hayuko? Kwa hivyo wewe kaa hapo uta anza wewe, ngoja lakini usubiri, keti usubiri niite wengine. Wewe ni Eric. Haya. Julius Matiguwany? Julius Matiguwany? Uko? uko karibu. Wewe ndio utafuatia. Peter Koech? Peter Koech? Mzee unge kuja pale karibu ndio ukiitwa uje mara moja. Zacheaus Sang? Mukae pale karibu na Mzee. Betty Kipkorir? Betty Kipkorir? Dada Betty Kipkorir? Alice Koskei? Alice Koskei? Alice mama Alice! uje pale karibu ukae chini ya mti ndio tukikuita ndio pale pale mama, pale juu. Uwe karibu. Haya kijana uanze nautaje jina nauendeleo

Mr. Eric Kerich : Kwa majina...

Com. Abubakar : Inua kidogo...

Mr. Eric Kerich : Kwa majina Eric Kerich, na mapendekezo yangu moja tuwe na boundaries, communal boundaries permanent halafu, hiyo ita reduce mambo ya tribal clashes. Hii watu wanapigana, kamawange kuwa na ma boundaries yao hawange kuwa wana pigana.

Com. Abubakar : Sawa...

Mr. Eric Kerich : Kwa watoto wale wana zaliwa free free mini na propose abortion iwekwe legalized halafu...

Com. Abubakar : inaudible

Mr. Eric Kerich : Ma-business tena makubwa, iwekwe, kwa kila ma-area wawe na hizo ma-business kwa sababu watu wote wata fanikiwa kwa kila area hizo.

Kwa madawa watu wapewe haki ya kutafuta dawa yeyote na atibu mahali hapo kwa sababu hata dawa kama hii ya ukimwi ingesha patikana lakini Serikali ili zuwua watu wenye wana weza kujaribu jaribu madawa haya.

Machinery iwe free kwa farm implements vitu kama ma-tractor nini, wa wekwe free kwa vile...

Com. Abubakar : Sawa [*inaudible*]...

Mr. Eric Kerich : Tena...

Com. Abubakar : Unataka vile vya kutumia katika kulima zi si wekwe tax...

Mr. Eric Kerich : Zi si wekwe tax..

Com. Abubakar : Sawa endelea

Mr. Eric Kerich : Inginge ni hii mambo ya squatters wapewe mashamba kwa vile wako in a free country wapewe wawe free nayo.

Com. Abubakar : Asante sana kijana uende pale... Julius Endelea Julius utaje jina na uendelee...

Mr. Julius Matiguwany : Thank you very much mimi naitwa Julius Matiguwany niko na mapendekezo machache sana. Kwanza office of the Ombudsman should be created in the District.

Com. Abubakar : Sawa...

muhimu sana kufikia hapa. Tumechukua maoni mzuri sana na tuna jua [*inaudible*] lime semwa kule, hili lime semwa pale na sote tunajua shida zetu zilizoko hapa Kenya na kwa hivyo maoni yenu hayatapotelea hapa. Munapo kua muna lazimishwa kutumia hii machine ni kwa maana tunataka hili machine iko kule iweze ku-record mambo yote ambao mume sema. Na wale ambao mume fika nyuma tuna taka kuwaambia ya kwamba hakuna neno hata moja ambalo lime baki. Tuta ya chukua haya maneno yote na tutaya tumia katika urekebishaji wa Katiba yetu. Ninataka kushuru wale wote ambao wamefanya uwezekano wa nyinyi kuitwa kuja hapa. Na shukuru juu ya shule hii kwa kutupa vifaa vyao ambavyo tume tumia, nataka ku shukuru Provincial Administration kwa kuweza kushirikiana na District Co-Ordinator wetu ili kufanya mkutano huu possible. Pia wale wa 3 C's, wale walio fanya Civil Education, na wale wote ambao wametusaikia kwa njia yeyote ndogo au kubwa nyote tunawashukuru mno. Sasa tumefika mwisho wa kikao chetu tulipo anza huu mkutano tulianza na maombi. Na tunapo maliza huu mkutano tunataka kumaliza na maombi ili Mungu atuwezeshe kwamba kazi zote ambazo zime fanyuwa maneno yote ambao mumesema ili atusaidie kwa kuweza kurekebisha Katiba yetu. Kwa hivyo ninataka kuita District Co-Ordinator, Mama unaneno la Bibilia unataka useme. Kwanza kabla mama haja sema hilo neno la Bibilia nataka kujua kama kuna ule amejitayarisha kutoa maombi [*inaudible*]. Ku naye? Okay tutamuita Mama aseme neno la Bibilia na pia atoe maombi ya kufunga mkutano.

Ms. Sophia Too : *En muguleldanyun ak en atebet ne u ni...*

Com. Ayonga : Kuna yule ambaye anaweza kutafsiria mama

Ms. Sophia Too : Yote najua Kipsigis

Com. Ayonga : Okay mama endelea.

Ms. Sophia Too : *Ogas o bichu... ng'alek cheu in.. ko ng'alek che kimwa Jeiso kole inorutechi nganaset ne kobe ak kotachak, kama wakiwapokea, si kor kokas toek korenyech anan kotachech.*

Yobe nganaset ne katachak obakach kaberuret. Lembeita ng'alechoto? Ng'anaset ne matachak oteiteite buiwet. Kibane noton okwek? Otebe. Kibane noton? Ne katachak en kiy nee? En amotwogik anan en buch?

Isoe muguleldanyun amun tomogere tuiyet en Poyytechnic ireyu ne kakile bwone toek agor ko moker kebai toek. Ki oger oin en yu ak koba buch kou noton.

Aini raini, kot ko kalel konyoiwon kat Jehovah, ene kirwogichu, yon kakile mi tuiyet ne u ni... Le kiasue kesomote agot en chu ki ame bik bik en ireyu, chu kiamate bik ak kolenen kimoche kinyaen ng'o, kimoche... kebendi sugul ak kelenji lagok, konetik kimoche kochangan chitugul, lakwet age tugul koib siling agenge si kinyo kikochi che kiyamech en koroni. Ii?

Kolyan si kobwa toek kotor koba... koberuretab Jehovah nitoni? Motogonu meet ne nyone o? Mokere bananda ne nyone ne bo kemeut ne bo kit age tuguli? Ko kimwa Jehovah Lembechi? Nganaset ne katachak koteben kaberuret, ne matachak.... Ko kirwogik ko ye kile bwone toek che echen che u chu koesy ogot kele onemun chi... ogot kinem chon kikekonor en yon tutukin tutukini asi kechopchi amitwogik bichu?

Kiami oin kotor komanda kou noton. Otoche koberuret inguni o en tuguchu ochobe? Akokochinige ng'alek che ochobe ole kimoche kole, kimoche kole amotorore Jehovah? Amoretiki bik che kimwa Jehovah kole oba emet komugul oamdechini ng'alechu?

Kabwa bichu, kaagas agot komi ne tobonu emon, tobonu ole loo. Ara karat amitwogik chito ne ka ruto? Kipsigisiek, moche kewalagen Kipsigisiek, ko kewalage amun ki atkinye ko kikikure chito konyo, kimokosirto chito en bi.

Interjection: (Inaudible)

Sophia Too: *Omwoe, nan amwa agenge si ketar, nan amwa korok.*

Com. Ayonga : [inaudible]

Ms. Sophia Too : *Ko noton ng'olyot ne kamwae ale obwat ak omwa, obwat ak osib Bible. Moweksei let ng'olyotab Jehovah ne kimwa. Motiyitiy kobwa bik kong'eten emon ak kor koba koweakta koberuret. Wee.*

Oini konchor emet, konyo kemeut. Kakile soini ko memi kiy bandet. Ne to kibwone ak kebai bik kwo ko biyongso.

Com. Ayonga : *Nataka, Mheshimiwa tulikuwa tume maliza habari ya ku kusanya maoni na mama alikua anasema maneno ndipo atupe maombi na nime mukataza aombe ningelipenda nikupe wakati huu usalimie watu na kama una jambo useme ndipo [inaudible] kwa hivyo [inaudible] uwasalimie na uweze kusema maneno mawili matatu.*

Mr. Charles Kirui : *Asante sana Commissioners ya Tume ya kurekebisha Katiba na kwanza nitasema pole nimechelewa kidogo lakini kuna kazi zingine ilini bidi niangalie siku ya leo kabla kupitia hapa. Nilikua nikitarajia pengine mutaendelea siku mzima katika area yetu hii. [inaudible] huenda pengine wamerithika na kazi yenu au hawakuwa na maneno mengi ya kutaja na pengine hivyo lakini na shukuru vile mumefika hapa kwetu na vile vile kupanga safari ya kuchukua maoni ya watu wetu. Inge kua jambo nzuri kama ninge pata nafasi ni ya sikia vile ambao yame wa gusia lakini ingawa hiyo nita taja machache.*

So ndio nitagusia haya maneno machache, lakini kabla sija ya gusia hayo. Pengine ninge fanya comment kidogo kuhusu yale ambayo yame kua ya kiendelea kwa magazetini au pengine kuhusu vile tume sikia report kutoka Commission yenu. Hivi majuzi

tumeambiwa Draft ya Constitution itakua tayari mwezi ya September na hiyo ikatupatia hofu kidogo sijui kama maoni yetu hii ambayo bado munaikusanya itapata nafasi ifike hapo ndani au pengine kuna Constitution ingine imekua tayari iko kwa mfuko. Hiyo pengine ndio utatueleza tukienda hapa mbele. Kwa sababu vile, pengine, au muko na speed, pengine muko na speed mzuri. Muna weza mukayamaliza haya yote kufika September muko na Draft. Shida tu ni bado tuna angaika vile vile. Sijui Draft itakua ni Draft yenu ambao mutaikagua ndio mfanye final copy au itakua ni Draft ya Bill ita kuja kwa Parliament. Kwa sababu kama ni draft ambayo ni yenu pengine ita chukua muda nyingine ndio ifikie kwetu. Na kitu tunge omba ni Review commission mutuambie kabisa haki na kinaganaga vile munaona hi programme inaweza kuendelea ndio tusiwe nana confusion katika vichwa vya watu wetu. Kwa sababu kama ikisemekana September watu wetu wengine wanafikiria Constitution itakua tayari September, Lakini pengine mungeeleza kama ni Draft hii Draft bado itatakiwa ifanyiwe hii, ifanyiwe hii, ifanyiwe hii, Constitution yenyewe vile munaona itakua ready muda gani. Kama ni September mutuambie ni hiyo September ndio itakua tayari kabisa. Kama utaona pengine ni December au ni January au May kama vile tulikuwa tuki soma kwa magazeti. Vile vile mutueleze vile munaona ikiwa Draft hii ni yenu ni itamfikia wakati gani mukifanya programme ambo hii Constitution hii kabisa itakua ni tayari. Kama ni mwaka huu au mwaka ujao. tungetaka tujue. Ndio watu wetu wakate shauri. Kwanza wanasumbuka tena kwa upande wa Bunge. Kwanza kama hii nina kubaliana na pengine maoni yenu ya kusema tusichukue muda ya bunge iambatane na muda wa kusahisha Katiba. Hiyo pengine ni mzuri. So tungetaka kujua kama hii Katiba itakua tayari mwaka huu ama tukate shauri tuende kura mwaka huu vile iko kwa programme itakua Katiba hii tunatumia hii mpya au ni Katiba ile ya zamani. Hiyo ndio tungetaka kujua kabisa ndio tusiwe tukisumbuka na kama naona viongozi kama sisi ndio hatujui hasa vile ina fanyika huko ndani ya Commission na hii mambo ya Programme ya kumalizika kwa katika lazima watu wetu wengi wanasumbuka zaidi. So ingekua ingefaa sana kama mungetuelezea kabisa. Tuseme tuko na Draft yetu au ni Draft ya nani lakini vile tunaona Katiba hii itakua ni tayari itakua ni mwezi fulani mwaka fulani. Halafu sasa tukiwa bunge au viongozi ndio tunaweza tukaambia watu wetu sasa munaona tukienda kwa mwaka huu tunatumia hiyo Katiba ya zamani. Hatuna shida ya kutumia Katiba ya zamani imetutumikia miaka arubaini hata wengi wetu vile tulikuwa tuki onelea hiyo Katiba ilikua ni nzuri ni vile tu viongozi wali kua wanaichukua wana sema iko mbaya au nini, viongozi wale wengine. Lakini kama tukisema tunataka Katiba mpya kabla ya kupiga kura ndio sasa tukate kauli tukijua ni Katiba gani. So hiyo tunataka Clarification.

Na niki ingilia upande ya maoni yangu. ningetaka tu kutaja kwa ufupi kwa sababu vile already niko na presentation ambayo nimeichora. Kuna mambo mawili ambao ni kama general. Vile na ona ni kama ina-determine, kwa maoni yangu, vile Katiba yetu inatakiwa iendeshwe au mukiandika iwe ni kama background iwe ni overriding issues, ndio ku, wakati munaitengeneza musifikirie sana. Kwanza ni upande wa ukabila. Ukabila si kitu kibaya kwa sababu sisi tuko makabila mengi Kenya hii. Ukabila ina kua mbaya kama group au kama kabila fulani anatomia ukabila yao kuangamiza wengine, Lakini ukabila kwa kanuni si kitu kibaya ndio Mungu ndio akatuumba akatupatia makabila tafauti tafauti. Shida tu ni katika jamii, tumetumia makabila kuangamizana na ndio na sema Katiba yetu lazima iwe ikifikiria ijulikane katika Africa hii, si Kenya peke yake ukabila ni kitu ya muhimu sana. Ina endesha siasa, ina endesha sababu zote kimila kinini, kabila ni jambo kubwa sana. Ukabila hasa vile nimesema si mbaya ni vile pengine inatumiwa na watu wengine vibaya. so inabidi tufikirie hii kabila tunaweza tukai weka Katiba yetu namnagani ndio kabila iwe jambo nzuri na iweze ikafanya kazi kuendesha mafanikio kuendesha development ya uchumi

yetu na ndio vile wengine wetu na mimi vile vile na simamia upande huyo sana. Na nimesema tuone vile tunaweza tukazitenganisha kidogo groups mbali mbali lakini tuunganishe vile vile. Sasa wakati tume uhuru wetu tumeinyakua tulikua na Katiba kama inge kaa vile ili kua nafikiri maendeleo ya area hii yetu inge kua ime endelea sawasawa katika kila area. Vile iko sasa ni areas zingine zime endelea zaidi waki tumia rasilimali ya area zingine. Kama tungeendelea na ile Katiba tulikua nayo ya jimbo ile ya majimbo mambo yetu ingekua inaendelea kwa utaratibu nzuri. Development would have been balanced. Vile imekua sasa imekua ni loop sided. Kuna area ime kula Kenya hii na sisi wengine bado tuna angamia, kuna area katika districts ziko katika njia za lami wakati mwengine kila mahali, lakini katika uhuru hii yetu mpaka hivi majuzi, hatukuwa na lami katika District hii tangu uhuru ili kua ni zile lami za zamani ile ya kuenda Kisumu na ile ya kuenda Kisii. Nyengine zote hatukuona na mpaka hivi majuzi. Lakini area zingine wamepatiwa hata, hata sijui kufanya hesabu. Lakini hiyo ni development ambao ingetukujia sisi zote kama inge kua shared kama kitu nzuri. Lakini kwa vile mali ya Kenya yetu hii ili enda kwa mfuko moja na mwenye alizichukua akisimamia hiyo mfuko ili kua ni ya area moja wakaangalia area yao, wakatusahau, na ndio tunasema inge kua ni jambo tupate kuji simamia hata tukiwa na ile kidogo yetu ibaki iwe ni yetu. Na kama kuna kitu ya katikati huko iwe ina kua distributed. Na ile jimbo neno majimbo majimbo vile tuna sema unajua jina hii ime haribika kutegemea na wakora. Wanasema majimbo ni kitu mbaya sijui majimbo ni hali ya kufukuza watu wa kabila zingine kutoka area wanakoishi. Ile majimbo najua mimi hii ni ya management ya Government kama mtu ametoka area ingine na anaishi katika jimbo hii hapo ni kwake. Hakuna cha kufukuza mwengine huyo ni mkenya. Lakini area hiyo itakua na management itakua na Government yake ya internal ya kuchukua mambo yakindani na kama tunge sikizana na kama tunge kua transparent katika matamshi yetu kila mtu Kenya hii wangeipendelea kadiri fulani ya regionalism na federalism hiyo ni kwa hawa wazee kama waki angalia upande huo wao waone to what degree hiyo inaweza ika enda, na weka, inaweza enda kabisa mpaka ina kua ile tunaita confederation ambao karibu kila area ina kua na Prime Minister, lakini kwa Kenya hii yetu nafikiri haita fikia hapo, kwa sababu sisi ni, bado ni nchi changaa na instruments za zile vitu zita hitajika kufanya kitu kama hiyo will be a bit too much kwetu. Lakini there should be some significant autonomy. Autonomy ile inaonekana ambao tunaweza tuka simamia mambo yetu. Central Government ama ile court ya central Government inagawanyiwa na inasimamiwa tumeona tumekua tukufanya hivi majuzi. Hata Mzee mwenyewe wakati alikua akiongea District Focus for Rural Development, hiyo programme ili kua undermined na watu wengine ambao hawa kutakia ma District kujisimamia. Hivi majuzi tume introduce kitu inaitwa latif. Na Councillors wetu wanajua sana. Na hii ndio imetuwezesha huko kwa mizizini grassroots wapate pesa kutoka Central Government. Hivi karibuni fuel levy, ku-distribute kwa Constituency na Districts hii ndio njia ku evolve mali kutoka Central Government na ienda kwa mashinani. Na hi ndio tunataka kuiona zaidi kwa kila pembe kwa kila wizara, ndio mali kutoka area zetu hizi na kwa Serikali ndio iweze ikafikia kwa wananchi na ichunguliwe kwa wananchi wenyewe. Watu wengine wana sema tukifanya jambo la majimbo ni ghali yaani hizo units za majimbo zitakua ni ghali lakini tuko fikiria already tuko na Provincial Administration, tuko na Provincial Commissioner, ako na Provincial heads yote. In fact there is already an infrastructure for Regional Government tuko naye hakuna kitu ya kuongeza. Pengine hata pengine itakua ni kupunguza. So already we have an infrastructure inaweza ikatumika pengine kama tukiwa na assemblies pengine kuta kua na gharama additional. Lakini ile gharama kama ita lead, au kama ita patikana muongozo mazuri, good management ile pesa ambao tuna weza tuka save tuna weza tukaichunga vizuri ndio itakua saved na itumike hapo because as of now tunajua katika Serikali kuna waste kubwa sana kuna upotovu mingi ya pesa kwa Serikali

kutokana na management ambao hai tush na kama tukipata hizi regional units, na regional units vile vile zitaenda kwa local authorities ambao zimewekwa nguvu ndio Serikali yetu inaweza ikamarika na fedha itumike. Neno lingine ambao ninge taka ku gusia ambao na sema hiyo ni background ikiwezekana kama hawa wazee wa commission wakiangalia ni mambo ya mashamba.

Katika Africa yetu hii, katika Kenya shamba ni kitu muhimu sana na tusipo ifanyia proper laws kuhusu upande wa mashamba tuta kua tume angamia. Kwa sababu ukiangalia katika Katiba yetu hii ni kama sura moja tu one section ina husu mashamba, inasema ukiwa ukona shamba yako haiwezi ikanyakuliwa bure bila ya malipo. Na inakwishia hapo ingine ni ya kueleza tu unaweza kuenda kortini kama ume chukuliwa shamba yako, na nini na nini. Lakini management ya shamba mambo yote hakuna. Ndio nimesema hata hiyo inahusu katika Constitution kuwe na Chapter kabisa ya kuongea maneno ya shamba na maneno ya umiliki. Maneno ya uhaki, wa shamba najua kuna Land Laws, Land Acts ambao ni tafauti lakini hii ikiwa ni sheria yetu ile inaitwa basic ya mwanzo kabisa naona inatakiwa iseme zaidi juu ya mashamba. Na ikisema juu ya mashamba vile vile tuki taja mambo ya compensation watu wetu wengi pengine mumugisia hapo walifukuzwa kutoka shamba zao. Hii ma kampuni ya chai ingine za miwa hata wengine ambao tunaita watalai waliondolewa nawakapelekwa mahali kwingine hawa watu walirudi wengine wana angaika katika town ya Kericho wengine walitolewa katika mashamba ya chai bado ni ma-squatter. Hao watu wata pata compensation lini jameni na ndio tukisema shamba yako isichukuliwe kabla bila compensation, hawajui compensation inanzia wapi. Inge enda mpaka ina mahali ili anzia kwa mbeberu mwenyewe. Tuna sikia wa America wale wanaitwa Red Indians huko Australia wanaitwa Aborigines sasa wanarudi kuuliza haki ya mashamba yao ambao wali nyakuliwa. Katiba yetu na vile ninaona inabidi itaje mambo haya na iguzie vizuri ndio tuweze tukamiliki mashamba yetu kwa haki. Shamba kama hii ya chai tunasikia na nimejaribu kuangalia katika sheria lakini vitabu inaonekana huko Commissioner of Lands hazipatikani kwa urahisi. Zengine sijui kama leases zao zinakwisha au zilikwisha au zinatakiwa ziongwzwe. Wakati hizo lease zilipo wekwa mara ya kwanza hakukuwa na compensation vile nimesema. Watu wetu tu walitolewa kwa mashamba yao bila compensation. Sasa kama tunaongeza hii lease tena si tunge tafuta wenyeji na kusema hii shamba yetu bado tunataka tena. Na hii ndio compensation yenu, tukikataa tukuseme hii compensation haitoshi iongezwe au tukisema hii shamba yetu sasa hatutaki kuikodisha tena tunataka irudi kwetu ndio irudi, lakini mambo kama haya inatakiwa iwe katika sheria zetu za kimuhimu. Hiyo ndio vile nilikua nikisema ni general comments. Na nikienda kwa mambo ya Constitution yenyewe ndio ninge taka kutajia kwa haraka haraka kabisa. Constitution yetu hii ya sasa iko na sura mingi karibu pengine kumi, sasa tukienda kwa chapter kama chapter one kimaelezo tu, chapter two inataja mambo ya executive President, Permanent Secretaries na vitu kama hizo, na vile nigeonelea katika Katiba yetu hii vile tuko nayo tuko na sheria kama nusu kwa kingereza kwa uchaguzi na zingine kama nusu ya kiamerica kwa vile tuko na Rais ambaye ni Executive na vile ninge onelea ni Katiba yetu ikiweza kana itawezekana na nafikiri itawezekana ni kuwe na Rais ambaye ata kua elected akiwa na mwenzake ambaye ni Vice-President. Yaani Rais awe na running mate ambao wata kua elected pamoja. Si ile ya ku-appoint. Na kama Rais akiwacha kazi kwa mambo fulani au shauri lolote kabla haja maliza hiyo term yake Vice-President aweze aka succeed na kuendesha mpaka amalize hiyo muda. Neno lingine ni uchaguzi wa urais vile tunafanya sasa tunafanya pamoja na Parliament na Local Authorities pengine tunaweza tuka borrow tuwe real kiamerica kama hiyo style iwe ni tafauti kabisa tuna ng'ang'ana na uchaguzi wana malizika halafu tuingilie hizi zingine ndio tern ya Rais isiunganishwe na ya Parliament. Kama hii yetu sasa kama term ya Parliament ina kwisha ndio unaskia vile tunasema kwa mambo hii ya Katiba, kama term yetu ikikwisha kwa January ya President vile vile itakwisha, lakini kama

ingekua ni tafauti term ya President inge kua independent na ile ya Parliament na sheria zetu inaweza ikatengenezwa iwe hivyo. Jambo lingine ambao pengine limetajwa ni wakati huu tunaelekea vile nina onelea ni inahitajika President apate 50% ya votes zote na vile ndio pengine itahitaji kama kuna watu wengi wana i ng'ang'ania hiyo kitu cha urais pengine tuwe na run-off kwa wale ambao au turudie kwa walili wako mbele hiyo ndio vile vile nime taka katika mambo ya ukabila na nini na nini ita fikia wakati ambao hakuna kabila inaweza ika pata 30% na achukue President peke yao. Mpaka waungane au wake pamoja na wakenya wengine ndio waweze kuifikia hiyo ndio na sema inge hitajika iwe na 50% minimum 51%, 50.whatever% kwa Provinces badala ya kusema 25% kwa hii au lile inasema nusu za provinces au regions kama tuta kua na regions at least half kama tuko nne at least half lazima ifike 50% vile vile. Again term ya President vile naonelea iwe ni ya miaka mitano vile wakati iko kwa Katiba na iwe ni two terms vile vile isizidi terms hizo mbili. Kwa maoni yangu vile vile, vile nimesema ku-cross au tuwe na ile ilio nzuri katika Katiba ya America vile tunajua tuna tumia America kama example tu kwa sababu kuna nchi zingine ambao wako na Katiba kama ya America lakini America ndio pengine inajulikana kwetu sana. Vile vile uingereza kuna vile vile ya ufaransa. Lakini vile na onelea kwa upande wa Parliament tunge kua na kitu kama ile ya uingereza, ambao wako na Prime Minister na Prime Minister uwe ina tokea ile chama ambao kime win elections to the majority of seats katika assembly wetu. Prime Minister itakua ingaa tuko na President na Prime Minister awe na powers ambaye ita kua specific kwa Constitution ndio kusiwe na confusion katika powers ya President na Prime Minister. Na Prime Minister vile vile ndio ata appoint kwa maoni yangu Ministers na Deputy Ministers kwa consultations au waki, consultations kwa kiswahili ni waki shirikiana, waki shauriana na Rais vile vile Ministers vile ninaonelea katika Ministries wasiwe na zaidi ya assistants wawili. Na zile Assistants ningeionlea iwe Deputy Ministers not Assistant Ministers. Na wawe Deputy Ministers ambao wana weza kusimamia kushika usuhukani kama Minister hayuko kwa ofisini. Vile tunao sasa katika Katiba yetu au ni kama practice. Assistant Minister hawezi aka shikilia Minister kwa mambo fulani kama Minister hayuko mpaka President ana appoint Minister ingine tutoka kwa wizara ingine awe acting kwa Ministry hiyo, Assistant Ministers katika uwezo walioko katika Katiba yetu hawawezi kuishikia usuhukani waziri ambao ame toka inje au ako safarini. Katiba yetu kama tunataka usimamizi nzuri katika Ministries, na watu ambao wana elewa mambo ya hayo ministries waka simamia ni upande wa Ministries tuwe na Deputy Ministers ambao wata simamia Ministers kwa kazi ya Ministries na attend Cabinet meetings on behalf of the Minister kama ni Deputy wakati huyo Minister hayuko ndio nimesema waitwe Deputy Ministers badala ya Assistant Ministers. Na ikiwa Assistant Minister akiwa sana sababu yake tume kua na shida shida fulani kuhusu hizo uwezo ya hiyo ofisi vile inakaa ingewekwa nguvu ndio tuka weza kusaidiana vizuri na Ministers wetu. Na vile vile ndio nataja Deputy Ministers wawe na specific responsibilities na inatakiwa ienda katika Katiba yetu kwa Ministries mpaka hata iki elekea mambo ya kuhusu Parliament na nini na nini wakihusika na mambo, na mambo hayo. Kuna katika section ishirini ya Katiba yetu jambo kidogo ambayo ina sema ma Ministers, Assistant Ministers au Vice-President kama wakitoka kutoka inje lazima waombe na wapewe ruhusa kwa barua na Rais tuliko sasa, Ministers na Assistant Ministers huwezi ukatoka inje kama ni kazi ya Serikali, kama ni jambo ya kibinafsi huwezi ukatoka bila kupata ruhusa ushughulike kwa nchi za ng'ambo, Minister hawezi akatoka na hii ime fanyika kwangu pengine mara mbili mara tatu. Kuna Delegation inatakiwa ipelekwe inje lakini kwa sababu Rais hakuna kuweka sahihi kwa barua huwezi ukatoka. Na Serikali yetu haiwezi ikawa represented kwa hayo mikutano na Minister au na Assistant Minister. Hiyo ni kama kazi ya Serikali inakwama, na inakwama kwa jambo unaona pengine hakuna haja. Vile kwa sababu ya vile Serikali inaendeshwa kingehitajika

tu ni ka-notice kwa Rais kwa ofisi yake kusema siku fulani nita kua na safari kama ni ya kibinafsi au ya kiserikali hiyo itoshe na iwe ni-acknowledgement. Hiyo ndio itarahisika, kama ni jambo inaonekana inafaa kuingia kwa Katiba. Lakini written notice in advance naona ni jambo ndio pengine inatatiza kazi ya Serikali saa ingine na tuna sumbua Rais sijui barua ngapi anapata kutoka Ministers, Assistant Ministers kile week, mpaka asome mpaka a barua iandikwe na aweke sahihi. Nafikiri Rais wetu ako na kazi kubwa kuliko ku-approve mambo kama haya. Na kwa upande wa appointment wa Ministers au Public Officers, Civil Servants, vile ningeonelea kwa vile hua tukifanya kazi katika Serikali yetu watu ambao ni Civil Servants unajua kuna ma Civil Servants hapa wengine lakini tume kua tuki tatizika na ma Civil Servants ambao loyalty yao ni ya upande mwingine. Hawafwati matakwa ya Serikali ilioko. Na ndio na sema inatubidi ma Civil Servants mpaka kadre fulani iwe ni kama Political appointments, ana kua appointed na Serikali hiyo ya wakati huo na Serikali hiyo ikitoka watoke na hawa. Hiyo ndio inafanyika upande za America ndio tukiwa na Permanent Secretary tunajua Permanent Secretary itafanya kazi ya Serikali hii. Tukiwa na Deputy Secretary, tukiwa na Directors tukiwa na Deputy Directors tunajua hii loyalty yake kwa Serikali yetu ndio inaenda sawasawa. Sio unasema mpaka label ya Deputy Heads of Departments yanatakiwa wawe akiwa appointed wakati President ana shika ushukani wanakua appointed na mwisho wa hiyo term kazi yao inakwisha. Na kama Serikali hiyo ikiwa elected tena pengine wata appoint hawa au wata appoint wengine. Inafanyika area zingine na inakua nzuri, hapa kwetu pengine inahitajika vile vile, sana sana kama tukiwa na hii mambo ya ukabila, ambao kazi ya Serikali pengine inakwamwishwa na tatu ambao wako na agenda ingine. So ningeonelea tuwe na technical people mpaka below Deputy Heads of Departments lakini Heads of Department there Deputies, Deputy Secretaries, Permanent Secretaries Directors wawe wanakua appointed wakati Serikali ikinigia hiyo Serikali ikitoka itoke na watu wake. Serikali mpya i-appoint watu wasimamie mambo ya Serikali, mambo mpaka upande ya chini no problem kwa sababu kutoka chini ya Deputy Heads iko Sub-Heads wengi wengi ambao wanakua ni technical people mpaka upande za chini mpaka kwa District hiyo wataendelea kawaida. lakini huko huko juu vile na onelea kama tutakua tukiendelea vizuri tena kuharakisha mambo ya kimaendeleo mpaka wafanyikazi wa Serikali washikane kabisa kabisa na viongozi katika Serikali, isipokuwa hivyo unakuta mambo inaharibika. Mtu anapewa cheo lakini loyalty yake ni mahali kwingine, na ndio na sema wafanyiwe hiyo halafu ndio nafikiri tunaweza tukafanya progress mzuri. Jambo lingine ambao nimeikuta katika section ishirini na saba upande ya hii nafikiri ili kua ina husu mtu moja hii prerogative of mercy katika mambo ya elections, election offence. Nafikiri kulikua kuna Mzee ame hukumiwa kortini siku ingine aka aambiwa huwezi kusimama kwa sababu umefanya Election Offence kwa sababu kama Election Offence ikifanyika mwenye ame fanya hiyo hana ruhusa husimama mpaka pengine nyakati zingine kutegemea na ile kortini amesema. lakini hiyo section ili kua introduced sub-section ili kua introduced in 1975 nafikiri wale ambao wazee kidogo watakumbuka. Ilikua ikatumiwa na President kumwachisha jamaa mwingine apate nafasi asimame tena, kwa sababu alikua amefungiwa inje. Ikaingia kwa Katiba na ikawani jambo ya mtu moja tu binafsi, nafikiri Katiba yetu haitakiwi iweikiongea maneno ya kibinafsi ni sheria ya nchi na jambo kama hili vile nimeona inafaa kuondolewa. Kwa upande ya Parliament ni machache tu nitagusia kuna mengi ambaye yange husu Parliament. Kwanza ni mambo ya nomination. Nomination vile iliingia katika Katiba yetu mambo ya kwanza ilikuwa ni kwa Serikali kupatia nomination watu ambao hawako pata representation katika mambo ya uchaguzi. Ilikua ni ya balancing kwa Serikali lakini ikafika wakati imekua ni mambo ya kisiasa tu mpaka sasa inagawanywa kama kuna twelve seats yanakua nominated inasema sasa inagawa proportionally kutegemea na ile seats kama ni ya Kanu ni ngapi kama ni ya Dp ni ngapi, imekosa maana. Vile

ingeonelea ni hiyo ifutiliwe mbali mambo ya nomination kwa seats ya Parliament au irudishiwe vile ilikua iwe kwa mikononi ya ile chama inayeongoza yaani kwa Serikali ndio iangaliwe kama ni kwa walemavu kama ni kwa upande ya kwa wanawake kama ni kwa upande hata ya racial minorities kama wahindi au wazungu ambao hawajiwezi kwa muda mrefu kufikisha mtu Parliament wanaweza kuangalia hivyo. So hiyo ndio pengine inaweza ikatumika, lakini kama inasema haifai ikae kwa mikono ya Serikali kuitumia kwa njia hiyo iondolewe kabisa kwa sababu ime kua ni wasted almost, ni makosa ile maana ambaye ilikua inatakiwa.

Neno lingine ambayo ningelipendelea ni tuwe na Katiba yetu ikubalie independent candidates, kama ni ya Parliament au ni ya Local Authorities kama mtu anataka kujisimamia bila kuungana na chama lolote hiyo ingekuwa na jambo nzuri, pengine ingetusaidia hawa watu wanapiga kelele kelele wana sema kuna Kanu . lakini wametokea upande mwingine, kuna sijui chama gani na wameenda wangefaa wawe na ni independent. Kwa sababu hii kitu imefanya hata tukawa na kitu cha ku chekeshwa, iko party ya independent candidates ndio ipate to go round hii Provision kusema hakuna mtu anaweza kujisimamia. Sasa kuna watu wakashikana, kuna jamaa mmoja akawa mwerevu sana akasema ninaanza chama cha independent candidates lakini chama cha independent candidates namna gani Bwana lakini wewe ingia kwa chama. Kama huko chama already wewe ni independent namna gani, so ndio na sema tusiwe na mambo kama haya ifutiliwe mbali hii mambo ya kusema lazima kila mtu awe ni kwa chama. Vile vile mambo ya expulsion and resignation au kutoka au kuondolewa kwa chama. Hii mambo ya chama ku expel au kutoa mwanachama yake kama ni Mp ame enda pahali ingine, iangaliwe nasema sheria hizo ambao ni section 39 katika Katiba hii na section 40 ziangaliwe ziwe clarified kwa sababu vile tukonayo sasa kuna confusion mtu ana sema ameenda kwa sijui Labour party au kitu gani na bado ako Parliament tuna sema aliingia na sijui Sdp au Mtu ya Kanu ana sema ameenda chama ingine na bado tunasema ni yetu, so ndio iwe clarified na tu iangaliwe. Mambo ya husiana na Parliament vile vile, Electoral Commission inasema nafikiri iko na members ishirini-na-moja. Ishirini-na moja kwa kamati ni kubwa sana. Sijui kama Review Commission pengine iko karibu size hiyo. Lakini pengine hii imetegemea kwa sababu kulikua na hii kitu inaitwa compromise at the end. Sasa kwa ku compromise tumeweka watu mpaka hata maana tena imepotea. There are too many kwa Electoral Commission ishirini-na-moja tunatakiwa nini jameni. Kisheria inasema for a committee to be effective iwe na nguvu naifanye kazi vizuri kusiwe zaidi ya watu kumi, in fact ile iko recommended ni kama watu sita hiyo kamati itafanya kazi kabisa, ita kua inafanya kazi muhimu. Lakini ikifika mahali na mpaka ishirini-na-kitu hiyo inakua ni shida so ndio naona kwa sababu ya iko balancing vile vile regions nini nini ndio na sema iwe kama kumi-na-mbili au kumi-na-tano. Kumi-na-mbili is what I would recommend as a maximum. Pengine kwa wanakamati wote ndio kazi iweze ikafanyika. Sasa na sikia si siri, tunajua hata katika kamati ya hawa wazee saa zingine wana zozana huko ndani. Ni kwa sababu wako wengi. Kama wange kua wako watu sita pengine, au watu kumi-na-mbili pengine hayo mambo hayange tokea lakini ndio vile nina onelea. Kwa upande ya constituencies review inatajika iwe intakiwa iwe ni miaka minane na isizidi kumi vile population hii ni kitu tumethuru kutoka sheria zingine vile population yetu inaenda speed sana ina-grow na vile vile watu wana hama town na nini na nini naonelea miaka mitano kati ya miaka mitano na kumi ndio inge kuwa ni ya jambo zaidi najua kuna sheria inakuja kwa Parliament au tunatarajia pengine ita ingia lakini inge tusaidia inge saidia nchi hii kama wazee wana rekebisha Katiba wange endelea na wa angalie upande huo. Vile vile Katiba yetu iko na katika hiyo section ambao ni section 42 iko na vile wange onelea constituencies yana weza yakatengenezwa kile nina sema ni pengine ni hawa wazee wangeifikiria waweke formula ambaye hata ukiangalia tumesema kuna viti mia mbili ukiona unajua ni kwa njia gani imefikishwa sijui District hii iko na tatu District ingine iko na nne District ingine iko na sita hiyo

ijulikane kwa sababu tukisema population ukiangalia hiyo peke yake haifuatwi sasa kama inge kua population pengine District zingine wako na sita wange kua na moja. So iko population iko kitu wanaita geography iko mambo mengine lakini tugesema hi na hi tukiunganisha uko na formula. Vile vile, vile naonelea kati ya ma-towns zetu na kati ya rural areas tusitumie population ambao ni sawa au inakaribiana. Sasa mambo ya town constituency hakuna kazi, pengine mwenye ako town anaweza akasema nimesema hivi kwa sababu constituency yetu ni ya rural constituency, lakini kwa town kweli kama na fikiri ni Starehe ambao Parliament iko member ya Starehe hataafiki Pumwani. Member ya Starehe hafiki duka za Westlands hafiki Kilimani kufika Kilimani umesha ingia Dagoretti au umesha ingia Lang'ata, au umesha ingia Westlands, so kama ni fifteen minutes au ni nusu saa ikiwa ime kua ni murefu. Member of Parliament ya Starehe ame zunguka constituency yake muzima ame maliza na ame rudi. Yetu hii pengine ni mwezi moja huwezi uka maliza, areas zingine hata pengine mwaka moja akizunguka tu bila kufanya chochote, hawezi akamaliza. Na tuna sema tuna represent hawa watu. Haiwezi ikawa sawa sawa. So ndio na sema ikiwezekana tu fanye proportion sababu tukisema ni population ya town iwe tafauti. Tuseme kama town kama Nairobi population ya constituency pengine iwe mara ishirini au thelathini ile ya rural constituency. Kama tuko na population ya one hundred thousand here pengine ya Nairobi iwe kama tukitumia hiyo kama million mbili before we can have a seat. Tena tunajuliza saa zingine City kama Nairobi ukiangalia kweli tunihitajika namna gani iwe na ma Mps wengi na wanafanya nini, kuna city Council wana tengenezwa barabara wanasimamia upande wa maji wanatengeneza maji, wana jenga shule, na wakati city Council wali kua ikifanya kazi vizuri na bado wanaweza waka fanya ikisimamiwe vizuri sasa ma-Mps wanafanya nini. Katika capital ya America ina ita Washington hawa kiti katika Parliament katika capital hiyo yao na kwa nini yetu tuna patia vitu nane jameni, kwa nini so ndio na sema inahitajika tufikirie na tuweke kwa sheria yetu tuseme ni proportional. Hatutake tuwawache bure but the best I can see hata ingawa wako na population karibu three million is to have two Mps ya Nairobi pengine moja ya Mombasa na town hizi zingine ndio watu ma-Mps wapatiwe watu ambao wanataka usaidizi, na vile vile tuna jua watu wanaishi Nairobi watu wanaishi ma-town zingine vile vile wako na ma nyumbani zao katika rural areas. Sasa wako na Mp ingine ya Nairobi na Mp ingine ya nyumbani. Na yule ambao unakaa nyumbani ukae kwa town uko na Mp moja, mwenye anakaa town ako na Mp mbili. That cannot be fair so ndio na onelea pengine iangaliwe upande ule upande huo. Jambo lingine dogo ni mambo ya urekebishaji ya Constitution sheria yetu vile iko katika section 47[iv] hii Katiba inasema kama Bill ya Constitution imetengenezwa iletwe kwa Parliament haiwezi kubadilishwa. Haiwezi kuwekewa amendment so ndio uichukue vile iko au uikatae na uirudishwe. That cannot be efficient, hiyo haiwezi ikawa ni, sijui mwenye alifikiria pengine alikua na saa zingine unajua ukora inaweza ikaingia mtu ana ingia mambo mengine bila kufikiria lakini hiyo pengine ndio ifikiriwe kwa sababu kama inaletwa Parliament na hakuna mabadiliko kazi ya Parliament ni nini. Na tunaipitisha tu yaani tunai-rubber stamp kama mimi nikiwa Mp yenu hiyo mambo kama hii Katiba sasa ikikwisha wakati ikikwisha badala tunaitumia hii kitu sheria vile iko haturuhisiwi, tunaweza tuka debate all the much we want tukapingana na nini na nini lakini hiyo mapingamizi au hiyo debate vile na sema ni hysteria una pingana pingana na kama mutapitisha itapita tu vile iko bila hata kuweka dot au alama yeyote katika hiyo sheria so ndio na sema inatakiwa iangaliwe. Maybe there should be some refinement na vile vile, vile nilikua niki nimesema kwa upande wa urais nili kua nimesema uwe na miaka mitano ambao pengine isfuatane na life of Parliament or term ya Parliament vile vile mimi ningelipendelea na pengine sijui watu wengine Life ya parliament vile vile iwe fixed wakati huu iko mkononi mwa Rais ana weza ku-dissolve kesho au keso kutwa au wakati mwengine wowote na kusema Parliament hii ime

kwisha, na ina kua ni mzuri Mzee Rais wetu na Mzee Rais wa zamani wali kua wazee watu wamekomaa, lakini kama ukipatie vijana kuendesha ushukani pengine anaweza aka sema kesho hii Parliament imeni sumbua watoke wote na ata kua na haki kusema hii Parliament iende nyumbani, ata sema tu saa hii Parliament imekwisha na ita kwisha na ndio tuna sema pengine kama tuna sema iko separation of powers au kuna tafauti ya powers upande wa kortini, upande ya Executive kwa President na ma officers wake, Ministers na nini ha huko upande wa Parliament upande wa Legislature, Legislature kama tunataka iwe na nguvu vile vile iwe na definite date kama zile tena na fananisha na zile za America unajua nafikiri sijui kama ni mwezi gani katika au tarehe gani kama first week on a Tuesday, *[inaudible]* second Tuesday of every November wana after five years iko kura ya Rais [four years] sorry ni four years kama ni hizo sasa tuna sema five tunaweza tuka sema, second Thursday, or third Friday of every five years baada ya elections na tuna kua na election ingine na inajulikana well in advance hakuna surprises kama kuna mtu anataka kusimama anataka kufanya campaign ya miaka miwili anaweza kufanya mwingine aki taka kufanya campaign ya mwezi mmoja anafanya, badala hii unaweza ukaanza campaign miaka miwili na pengine unakwisha njiani hapo. Kura bado itaitwa una jua area yetu hii kulikua na watu wanafikiria tuta kua na elections May mwaka huu akaanza campaign mwaka jana sasa sijui wako wapi pengine bado wako wanaendelea, lakini kama tunge jua kwa ki sheria tuna jua tarehe fulani kama ni mwaka huu every five years lazima kukuwe na elections ya Parliament au elections ya President ndio inakua very very transparent so this is what I would encourage kwa upande ya President kwa upande ya Parliament, lakini vile na sema hakuna haja zifuatane sana ziwe ni tarehe hizo ya Parliament na ya President vile ninaona hata inafaa zaidi uchaguzi wa President ifanyiwe pengine baada ya ile ya Parliament na mambo kama hayo. Neno lingine ambao iko kwa upande ya Chapter five ni mambo wa vile tunaita fundamental rights and freedoms of the individuals the right to associate the right of expression the right of mambo mambo mengine hapo ndio vile vile iko na right ile ya property ya mashamba na nini ambao nime gusia ile ya mashamba kuona kwangu haitakiwi kuwa section kidogo katika Chapter hii ni jambo kubwa na inatutaliza maisha yetu inatakiwa Chapter yake yenyewe naitungwe mambo yote ya kuhusu mambo ya mashamba na kumiliki lakini vile vile kume tajwa mahali kwingine mtu ambaye anaweza kusimamia najua Serikali yetu ina jaribu sana kuna kortini kuna nini lakini mambo ya kortini kama umeangamizwa saa zingine inakua ni ghali kwa mwananchi ingetakiwa kuwe na ofisi na katika nchi zingine pengine zime endelea kidogo ako na ofisi inaitwa ofisi ya Ombudsman a Commissioner ambaye kama umeangamizwa shamba yako imenyakuliwa au umekataliwa kufanya mkutano au kanisa yako imekataliwa kuwekwa register au mambo kama haya ndogo ndogo ambaye yange kuumiza kwenda kortini una weza kwenda kwa ofisi hiyo naiangaliwe na mtu anaweza akajisimamia na ndio na sema katika Kenya yetu hii tunahitaje level kama hiyo kwa wakati huu. Nafikiri tume komaa kisiasa na kimaendeleo tunahitaji ofisi hii na kuwa na ofisi za kutosha, watu wetu wanaweza kwenda huko na malilio kama wame nyanyaswa area mbali mbali, kama ni sisi viongozi tume wa nyanyaswa au ni vitu kama hizi vile vile ndio tuwekwe kwa miguu yetu ndio tuangalie mambo haya vizuri. Neno la mwisho ambayo nitaigusia kwa sababu siwezi nikazitaja zote ni upande wa Citizenship au uraia, katika Katiba yetu nikama inakalia sana upande ya wanaume sijui kama pengine mulikua mumetajiwa upande hiyo, so ndio na sema inafaa watu wetu wote kama ni wanawake au ni mwanamume kuweza kupata uraia au kama ukioa kama mkenya sasa uowe bibi kutoka nchi nyingine huyo bibi yako anakua raia ya Kenya, huyo bibi yako anakua raia bila wasiwasi hata hakuna question, lakini kama mtoto wako ambao ni mkenya akioa mgerumani au mahindi au muethiopia aje hapa kupata uraia mpaka atazunguka na kuzunguka so hiyo nafikiri ndio kosa mahali fulani. Nyakati hizo pengine ili kua ni sawa

pengine ili kua ni nzuri, vile vile katika hiyo ndoa yao msichana mkenya na mgerumani au mtanzania akizaa watoto hao watoto wa haya hawawezi kua ni wakenya lakini kama inge kua ni mwanamume ama oa mtanzania watoto wanakua wakenya kwa urahisi. Hiyo tena inakua ni ubaguzi. Kwa mambo mengine ambayo pengine wa kina mama wame ikazia siwezi nikaingilia sana upande huo lakini sana na kaza upande wa uraia ambaye naona wanawake wetu wame fagiliwa sana. Kama mtoto tunatuma ma vijana wetu waende wakasoma ng'ambo pamoja na wavulana wengine wanaweza wakarudi wameoana na watu wa nchi zingine kama ni mvulana mtoto ana kua mkenya kama ni msichana inkua ngumu na one turekebishe sheria upande huyo. Kwa hayo machache au marefu na sema asanteni sana kwa kunisikiza. Thank you very much.

Com. Ayonga : Mweshimiwa Kirui tunataka kuku shukuru sana nathani kazi yetu haingelikua complete without having your presentation. Umefika and in a very systematic way ume present your paper ambaye itakua very useful katika kazi yetu ya kurekebisha Katiba. Nakushukuru sana sana kwa kuweza kutupa hii presentation yako. Watu wako hapa wame changia sana na ume tupa presentation ambayo itatu saidia mno kwa kufanya kazi yetu ya kurekebisha Katiba. Nataka nikuhakikisha ya kwamba wakati ambapo umechora jina yako hapo presentation yako ita kuwa registered as a document ambaye itatusaidia katika kurekebisha Katiba. Na ambavyo utakua mmoja wapo ya wale ambao watakao kua katika national conference utaona kwamba mambo yako yamo na pia itatusaidia pia kwa kurekebisha Katiba. Na kushukuru sana Bwana mweshimiwa na tume kuwa na mkutano mzuri ambaye nili kua nimesha ambia watu wako hapa asubuhi kabla huja fika kwamba our meeting with your people of this constituency has been very fruitful. Na kama hakuna mengine... Nataka yule mama wetu ambaye alikua amejitolea ili aweze kutotolea maombi, mama ningelipenda sasa usimame tena [inaudible] sasa itakua ni maombi, mama alisha kua amesha sema [inaudible]

Ms. Sophia Too : *Itoche Kipsigis o anan itoche achon? Toche alak tuguli. Kongoi Jehovah amun saini Kakenyoru. Awekyini kongoi Mheshimiwa ne momi kit ne kerge ne ndomo saisiek che begu amun ka ng'alekab raini ko kakilitite ng'alekab ole kibetitoi en ngweny.*

Kongoi en ng'alek che kakosomonwech, en sobenyin, ak en tuguk tuguk ak ole kimoche kesopten Kenya.

Osoe kityo, lakini nyigis muguleldanyun Kipsigisiechu; olenyigisindo muguleldonyun ko kin keget tondet koroboni koiyan kome koronon, noton ne iimon, mache agot kelenjon lianen kowendi chito en koroni? Matomwa. Asoe Jehova, kose Jehova, kose Jehovah chotoni? Mokose Jehovah. ngoja kwa nini sisi watu wa Mungu sisi nataka omba Mungu halafu nabariki sisi, si hata nchi imekauka, kiangazi namaliza sasa dunia yetu, kila siku hatu, karibu watu na taabika kwa jua kwa nini kwa maana watu hapana omba Mungu kwa amani ya Mungu kila mtu na chukua kitu na fanya namna gani namna gani halafu nasema kama na sema omba Mungu ni kidogo. Omba omba kidogo, hii kitu inasema nini. Jseu ali sena kwa siku ya hukumu kama mini na keti kiti nita gawa watu kenda upande hii na upande hii kwa maana mimi nilikuja kwako wewe na fukuza mimi, mimi nilikua mugonjwa hapana ona mimi, milikua njaa, nilikua uchi, nilikua namnagani hakupata kwenda njia yenu na hii njia yenu.

Interjection: (Inaudible)

